# Nipashe

Jumatano Aprili 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581278

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Mchangia uhuru aliyekimbia nchini miaka michache baada kuwa waziri

Ukurasa 12

Miaka 39 bila ya Sokoine, ujasiri na uchapakazi wake ukibaki kuwa alama

Ukurasa 13

siasa

JUMATANO APRILI 12, 2023 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Wadau watoa ya moyoni, mahakama kukataa 'wagombea bila kupingwa'

Ukurasa 13

Rais alivyotumia Ripoti CAG kuthibitisha kukubalika, uwazi, uwajibikaji kwa umma

• Kilichoamuliwa TRC yawa darasa aina yake

Na Mwandishi Wetu

Ingumu sana kwa wataalamu wa siasa wanaeleza katika namna ya kutenganisha siasa na mwenendo wa uchumi na mara zote huwa zinategemeana. Siasa mara zote huamua jambo, huku uchumi ukiwa unaendesha hali halisi na maisha ya kila siku.

Wanasiasa hushikilia nyendo hizo, nguvu kuu ikiegemea penye undani wa uchumi. Nchini hadi sasa, kuanzia maisha ya kijamii na hata kisiasa, mada inayotawala kwa kiasi kikubwa ni Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22, iliyotolewa siku chache zilizopita. Ni suala la fedha na uchumi, ikikamata nguzo ya kisiasa nchini.

Mara tu baada ya ripoti hiyo ambayo akamwasilishia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye naye anatolea ufafanuzi wa majibu na uamuzi, pasipo 'kuyakopa' bali akayafafanua kwa kina undani wake na mwelekeo wa kiserikali.

UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!

TZS. 544,830,140

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Wamiliki ardhi kuanza kupokea bili kupitia simu

UKURASA 3

# Bulaya aibua tena kikokotoo bungeni



• **Asema** 33% ni maumivu kwa wafanyakazi, adai wana kinyongo nacho *Ukurasa 2*

## Othman apendekeza kiwapo chombo rasmi kusimamia haki jinai

UKURASA 3



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman akitoa maoni yake mbele ya Tume ya Rais ya kukusanya maoni ya Maboresho ya Taasisi za Haki Jinai Tanzania, Jaji Mkuu mstaafu Mohammed Chande Othman (wa pili kushoto) na Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue (kushoto), ofisini kwake Migombani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMKRZ**

# CAG aibua utata mkataba wa ubia kibiashara NHC

UKURASA 2

**MICHEZO** **BALEKE: KIWANGO CHANGU BADO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo na Kinondoni, Boniface Jacob (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es salaam jana kuhusu uchambuzi wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Halmashauri tano za mkoa huo na kutaka viongozi waliosababisha hasara wachukuliwe hatua za kisheria. Kulia ni mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Martin Masese na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la chama hicho, Jimbo la Ubungo, William Mwangwa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Bulaya aibua tena kikokotoo bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Easther Bulaya, ameliamsha upya Bungeni sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu, akisema wafanyakazi bado wanalia na wanafanya kazi kwa kinyongo, kwa kuwa asilimia 33 inayotumika si haki yao.

Bulaya, wakati anachangia jana bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, alisema maisha ni magumu na wafanyakazi wanalia, wanafanya kazi kwa kinyongo.

"Tusitengeneze mgomo baridi. Hawa ndio wanaoenda kutekeleza miradi ya maendeleo. Najua mnasikia, najua mmeona na najua mkiamua kulifanya jambo mnaweza. Bado asilimia 33 si haki yao. Maisha magumu, wafanyakazi wanalia, wanafanya kazi kwa kinyongo.

"...Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa), tunajua wewe ni mnyenyekevu, tunaomba watumishi watimize wajibu wao. Mifuko ya hifadhi ya jamii, madeni yalipwe, watumishi pesa zao kwa mujibu wa sheria, michango ipelekwe kwenye uwekezaji.

"Kuwe na tija, ifanyike tathmini ya kina ili hizi fedha za hawa watumishi wa umma ambao ni wastaafu watarajiwa waje wapate haki zao," alisema.

**MAJIBU YA KINA MKULANZI**

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mkulanzi uliofikia asilimia 75, Bulaya alisema wanataka majibu ya kina kwa sababu kuna fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii zimewekezwa kwenye mradi huo.

"Tunatataka majibu ya kina; hapa kuna fedha za mifuko zimewekezwa. Je, tathmini ya kina ilifanyika? Maana ripoti mbalimbali za CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) zimeonyesha hapa pametengeneza hasara ya Sh. bilioni 11 sawa na asilimia 21 ya mtaji uliowekezwa.

"Na moja ya sababu inasemekana, kuna ucheleweshaji wa mashine. Sasa ukienda ya mwaka huu, inasema hiyo mashine aliyepewa tenda ya kununua mtambo wa kutengenezea kiwanda cha sukari ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), wapi na wapi? Kwa nini haikuwa TEMESA (Wakala wa Umeme na Ufundi), kwa nini haikuwa Wakala wa Uagizaji wa Vifaa Serikalini? Why TANROADS. Barabara na sukari wapi na wapi?

"Na hapa kuna fedha za Kimarekani takribani milioni 50.8 na inasemekana mbali na huu mkataba, Mkulanzi hawajashiriki mpaka kuweka saini, kila kitu walifanya TANROADS," alisema.

"Kuna nyongeza ya Sh. bilioni 11 na hatujui kwamba Mwanasheria Mkuu alithibitisha kwa mujibu wa Kanuni ya 59, Kifungu (i) cha Manunuzi. Tunataka majibu ya kina. Haya tunayasema kwa sababu tunataka hatua zichukuliwe. Watu wasiichukulie serikali poa, watu watimize wajibu wao na hizi ni fedha za wastaafu wetu," alisema.

**HASARA BIL. 4/-**

Katika mchango wake kuhusu uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii, Bulaya alisema Kiwanda cha Ngozi cha Kilimanjaro, kimepata hasara Sh. bilioni nne.

Alisema hizo ni fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii na katika malengo yao. Kiwanda hicho cha Kilimanjaro kilikuwa kimepanga kuzalisha jozi za viatu milioni 1.2 lakini wakazalisha 11,354.

Kwa mujibu wa Bulaya, kiwanda hicho pia kilikuwa kimepanga kuzalisha jozi za viatu, soli za viatu 900,000 lakini kikazalisha sifuri. Kilikuwa kimepanga kuzalisha bidhaa za ngozi 48,000 lakini kikazalisha 224.

Kana kwamba haitoshi, akasema kiwanda hicho kilikuwa kimepanga kuzalisha ajira 300 lakini kikazalisha 79 na malengo hayajafikiwa huku akisisitiza huo ni usimamizi mbovu kwenye fedha za wastaafu zinazowekezwa kwenye viwanda, wakati hayo yanafanyika bado mifuko iko hohehae.

**BIL. 129 ZA MICHANGO**

Vilevile, akichangia kuhusu Mfuko wa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Bulaya alisema yako mashirika manne hayajapeleka michango takribani Sh. bilioni 129 kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Wakati hayo yanaendelea, kuna mamlaka ya serikali za mitaa 133 hazijapeleka tabribani Sh. bilioni 119, maslahi ya mishahara na posho za wafanyakazi hazijalipwa. Pia kuna mashirika nane hayajalipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi na madeni mbalimbali takribani Sh. bilioni 5.8, bilioni 2.2 ni malimbikizo ya mishahara. Pia kuna mamlaka za serikali za mitaa 76 hazijalipa Sh. milioni 309 za mizigo za wastaafu 223," alisema.

Kadhalika, Mbunge huyo alisema katika ripoti mpya ya CAG, PSSSF imesema ukwasi uko asilimia 22 kinyume na sheria cha asilimia 40.

"Mwaka jana nimesema na leo narudia, wakati hizi pesa zinaendelea Sh. bilioni 1.5, pesa za muda mrefu hamjalipa kwenye mifuko iliyoahidiwa na Waziri wa Fedha, atalipa kwa hati fungani,

"Pia Waziri wa Fedha PSSSF mmelipa Sh. bilioni 767 pesa za wastaafu, kiinua mgongo chao zaidi ya pato walilo nalo. Kuna mwaka walienda kukopa kwenye maeneo mengine kiasi walicholipa ni kingi kulingana na mapato na michango," alisema.

**TAARIFA KWA UMMA**

KUFUATIA TANGAZO LA AJIRA NAFASI 572 LA TAREHE 18/3/2023 LENYE KUMBUKUMBU NAMBA 9/274/3/M/167 NA JINGINE LA WITO WA USAILI LA TAREHE 06/04/2023 YANAYOSAMBAA KATIKA MITANDAO YA JAMII HAPA NCHINI.

**MOUNT MERU PETROLEUM LTD** INAPENDA KUUTAARIFU UMMA KWAMBA MATANGAZO HAYO YOTE MAWILI SIYO YA MOUNT MERU PETROLEUM LTD NA KAMPUNI YETU HAIHUSIKI KWA NAMNA YOYOTE NA MATANGAZO HAYO.

**UTAWALA.**

## CAG aibua utata mkataba ujenzi NHC

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini mkataba wa ubia kati ya Kampuni ya Al-Karimo Investment na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) wa ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la kibiashara na makazi, Dar es Salaam ambao haujakamilika kwa miaka 17, huku mbia akijumuisha kiwanja chake kwenye mradi bila ridhaa ya NHC.

Aidha, uchambuzi wa ripoti hiyo umebaini kuwa mbia alitumia kiwanja chake kuchukua mkopo Benki ya Kimataifa ya Biashara (ICB) kwa ajili ya ujenzi wa mradi lakini alishindwa kulipa mkopo huo na deni limefikia dola za Marekani milioni 2.35 (sawa na Sh. bilioni 5.47).

Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ya Mwaka 2021/22, inaonyesha kuwa usimamizi usioridhisha wa mkataba huo wa ubia wakati wa ukaguzi, kasoro kadhaa zilibainika.

Kasoro hizo ni pamoja na mbia kujumuisha kiwanja chake kwenye mradi bila ridhaa ya NHC na ujenzi ulifanyika kwenye viwanja vitatu, badala ya viwili vilivyotolewa na shirika.

Mwaka 2004, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), liliingia ubia na Kampuni ya Al-Karimo Investment Limited kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo kwenye viwanja viwili vya NHC kwa faida ya kibiashara na madhumuni mengine kama yalivyokubaliwa kwenye mkataba na mbia anayefadhili mradi huo.

Kutokana na usimamizi usioridhisha wa mkataba huo wa ubia, CAG amependekeza NHC ifanye usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha na wa mara kwa mara katika uwekezaji wake wote wa ubia.

Aidha, amependekeza NHC iwasiliane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kupata ushauri kutokana na kasotro zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkataba huo wa ubia na hatima yake kwa maslahi mapana ya taifa.

Kuhusu kutokufanya mapitio na kutoidhinishwa kwa kiwango cha kodi ya wapangaji, CAG amesema NHC haikufanya utafiti wa soko ili kuhuisha viwango vyao vya kodi.

Kwa mujibu wa CAG, hali hiyo inasababisha kutoza kodi kwa kiwango cha chini na kupoteza mapato. Kiwango cha sasa cha NHC kinachotumika kiliidhinishwa mwaka 2011 na hakijafanyiwa mapitio ya kuzingatia mabadiliko ya kiwango cha mfumuko wa bei, na hali ya soko kwa miaka 10 iliyopita.

Kwa hali hiyo, CAG amependekeza kuwa Shirika la Nyumba la Taifa, lifanye utafiti huru wa soko ili kubaini kiwango cha sasa cha kodi ya soko.

Pia shirika linapaswa kupata idhini ya bodi kabla ya kutumia viwango vipya ili kuepuka kutoza kodi chini ya kiwango cha soko la sasa na kupunguza mapato ya shirika.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mradi wa Barabara ya Mabasi ya Mwendokasi (BRT 3), Mhandisi Barakaeli Mmari (kushoto), wakati alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara inayotoka Gerezani hadi Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Wamiliki ardhi kuanza kupokea bili kupitia simu zao

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema wamiliki wa ardhi nchini wataanza kupokea bili za kodi ya pango la ardhi kupitia simu ya mkononi.

Dk. Mabula alisema hayo jana wakati Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliposimama kwa muda kuzungumza na wananchi wa Hungumalwa, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza, ikiwa ni mwanzo wa ziara yake ya siku tatu mkoani humo.

"Ninapozungumza sasa mikoa kumi tayari imeunganishwa katika mfumo na tutaanza kupata bili zetu kupitia simu ya mkononi hivi karibuni maana watu walikuwa wakihoji kama maji waliweza kwanini ardhi wasiweze," alisema Waziri Mabula.

Dk. Mabula alisema, kwa sasa kuna wataalamu 26 wanaboresha mifumo ndani ya wizara hiyo lengo likiwa kuhakikisha mifumo ya wizara inaimarika katika masuala ya malipo ili kuwawezesha wamiliki wa ardhi kuondokana na changamoto za ulipaji kodi ya pango la ardhi.

"Napenda niwahakikishie wananchi wa Hungumalwa, Kwimba na wana Mwanza kwa ujumla kuwa zile kelele za ardhi zinaenda kuisha kwa sababu mama Samia ameiwezesha wizara," alisema Dk. Mabula.

Aidha, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amefungua nchi na kuhitaji kuwa na wawekezaji na kubainisha kuwa wawekezaji lazima wakute ardhi zipo na zimepangwa na kuwekwa kwa uwekezaji.

"Niwaombe katika kutenga maeneo ya uwekezaji lazima tuhakikishe yametambuliwa na yanamilikiwa lengo mwekezaji akija asianze kuvutana na wananchi, halmashauri na serikali ya kijiji husika iwe imefanya utaratibu wa kulitambua eneo na kumiliki," alisema Dk. Mabula.

# Makamu Othman apendekeza chombo rasmi kusimamia haki jinai

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuna haja ya Tanzania kuitumia fursa ya kuundwa Tume ya Rais ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, nchini kupendekeza kuandaliwa mfumo utakaounda chombo rasmi na kuandaa sera bora itakayosimamia vyema kimamlaka masuala yote ya haki jinai nchini.

Othman aliyasema hayo mjini hapa alipokutana na Wajumbe Tume hiyo iliyofika ofisini kwa Makamu kupokea maoni yake kuhusu maboresho yanayohitajika katika taasisi za haki jinai na mfumo wa mahakama Tanzania.

Alisema Tanzania kwa sasa inaonekana hakuna mfumo na sera rasmi za kusimamia taasisi za aina hiyo na kwamba ni jambo jema Tume hiyo ikapendekeza kuundwa mfumo rasmi na chombo kimoja chenye mamlaka kubwa pamoja na kuandaliwa sera itakayosimamia masuala hayo kwa wepesi na kusaidia upatikanaji wa haki kwa jamii.

Alisema kwa sasa utaratibu uliopo Tanzania ni upungufu mkubwa ambao hauna uwezo na hauoneshi kuwapo utaratibu bora utakaosaidia watanzania kuendesha kwa wepesi taasisi na mfumo huo sambamba na kuzuia kujirejea rejea kwa makosa ya jinai ya aina mbali mbali yanayotendeka nchini.

Pia, alisema maboresho mbali mbali yaliyofanyika katika mfumo wa sekta ya sheria nchini bado hayajakidhi haja na matarajio ya nchi kuwa na chombo kimoja kinachosimamia masuala yote muhimu ya haki jinai kwa kuwa yaliyofanyika yalizingatia zaidi urekebishaji wa kitaasisi kuliko mfumo unaohitajika sasa.

Alisema Tanzania itakuwa imefanya jambo kubwa iwapo itatambua inahitajika kujenga upya mfumo na utaratibu wake wa haki jinai ili kuondoa tatizo la sasa lililopo.

Kadhalika, mfumo wa sasa pia unaruhusu makosa makubwa kutendwa na watu wenye nyadhifa kubwa huku utaratibu na uwezo wa upelelezi wa polisi ukiwa dhaifu kutokana na kujengwa kisiasa kuliko kiuweledi zaidi, jambo ambalo athari inarudi katika kuzuia na kupeleleza makosa mbali mbali ya jinai na hivyo kulazimika kutumia maelekezo ya viongozi wa siasa.

Alisema mfumo huo wa polisi kupokea maelekezo ya kisasa inalifanya jeshi hilo kukosa na kujenga weledi katika upelelezi wa makosa huku kazi hiyo ikiwa ni ya kitaalamu zaidi kuliko ya siasa.

Kutokana na hali hiyo amesema kuna haja ya kutathmini Idara za upelelezi katika Jeshi la Polisi kwamba iendelee kubakia ndani ya jeshi hilo ama iwe mamlaka mbali na jeshi la polisi linaloweza kufanya kazi zaidi ya kupeleleza kwa weledi mkubwa makosa tofauti ya jinai.

Othman alisema hasa katika vipindi vya uchaguzi, mfumo ulipo sasa wa polisi huendelea kupokea amri za wanasiasa na hivyo kuwafanya polisi kuendelea kutumika vibaya kinyume na malengo na matarajio ya jamii ya watanzania jambo ambalo ni tatizo kuwapo hali hiyo.

Kuhusu Taasisi na Mamlaka kama za kuzuia rushwa , Tume ya Kuzuia na Kupambana na madawa ya kulevya na mamlaka nyingine za namna hiyo, alisema kwa mazingira ya Tanzania ni vyema kuundwa kwa kuungwa pamoja chini ya chombo maalum kitakachokuwa na uwezo wa kitaalamu na rasilimali za kutosha za kushughulikia mambo maalum ya namna hiyo chini ya maadili na kuweka wepesi zaidi kiutendaji.

Eneo jingine alilolizungumzia ni kuhusu masuala ya kitaalamu kama vile kwa Mkemia Mkuu, madaktari hali ilivyo sasa hawakutengenezwa kwenda kusaidia katika upatikanaji wa haki mahakamani lakini hutazama eneo la utaalamu zaidi katika viwango vyake vya Kitaasisi visivyomunganiko huku kukiwa hakuna mamlaka ya juu zaidi ya kusimamia zaidi.

Mwenyekiti wa Tume hiyo Jaji mstaafu, Mohammed Chande Othman, alisema Tume hiyo inaendelea na kutekeleza jukumu lake la kukusanya maoni na taarifa kupitia wadau mbali mbali wakiwamo viongozi, taasisi za haki jinai na wengine kwa njia ya mikutano, madodoso pamoja na maandishi ili kuweza kukusanya maoni na kuishauri serikali namna bora


International School of Tanganyika
Challenge | Support | Inspire

Elementary Campus: elementary@istafrica.com, +255 684 228 882/5, United Nations Road
Secondary Campus: secondary@istafrica.com, +255 787 992 778/98, Haile Selassie Road
Dar-es-Salaam, Tanzania

## INVITATION FOR BIDS

Bids are invited from interested registered, competent, reliable and licensed suppliers/dealers to provide the under listed goods and services for the year ending 31st July 2024.

| S/N | Category No. | Description |
|---|---|---|
| 1. | Category 01 | Maintenance Materials |
| 2. | Category 02 | Consumables and Cleaning Materials |
| 3. | Category 03 | Stationeries |
| 4. | Category 04 | Staff Welfare Supplies (Sugar, Tea, Coffee & Milk Powder) |
| 5. | Category 05 | Timber |
| 6. | Category 06 | Supply and Servicing of Fire Extinguishers |
| 7. | Category 07 | Fumigation |
| 8. | Category 08 | Cesspit Emptying |
| 9. | Category 09 | Electrical Appliances (Fridges, Cookers & Air-conditions) |
| 10. | Category 10 | Motor Vehicle Tyres & Battery |
| 11. | Category 11 | Motor Vehicle Oil & Filters |
| 12. | Category 12 | Motor Vehicle Spare Parts |
| 13 | Category 13 | Motor Vehicle Bus Hiring |

**Conditions:**

- Bid document(s) will be emailed to the bidders on payment of **TZS. 25,000/=** payable per bid category. Payments should be made to the Billing Department located in the Administration Building (Gate #5), off United Nations Road, Upanga, between 10.00 am to 1.00 pm Monday to Friday. Bidders will need to provide the School with the email ID at the time of making payment. Once payment has been received, bid documents will be emailed by the following working day.
- Bids should be emailed to **bids@istafrica.co.tz** latest **by 2 p.m. on Friday, May 5, 2023**. No bids will be accepted after this time. In addition, bidders should attach scanned copies of certificates of registration, business license, TIN/VAT certificates and User Identification Number certificate (for VAT registered suppliers). On submission of the information, the bidders would receive a confirmation that IST has successfully received their bids.
- The School is not bound to accept the lowest or any bid and reserves the right to reject all or any of the bids received.

# LATRA yafungia leseni madereva 30, mabasi 27

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesitisha leseni za mabasi 27 yanayofanya safari mikoani huku madereva 30 nao wakifungiwa leseni zao.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema sababu za kuchukua hatua hizo ni kutokana na madereva kuendesha kwa kasi na kuchezea mfumo wa kufuatilia mwenendo wa gari (VTS), hivyo kusababisha usitoe taarifa au kutoa kwa kuruka ruka.

"Kuna baadhi ya mabasi ambayo baada ya wataalamu kufanya uchunguzi, waligundua betri za vifaa vya VTS zimeharibiwa na mifumo yake ya umeme kubadilishwa.

"Kadhalika, kuna basi ambazo zimekutwa zikiwa na mfumo wenye swichi inayotumiwa na dereva kuzima na kuwasha na kuna ambazo zimebadilisha mfumo na kutuma taarifa za uongo kwenye kituo chetu cha ufuatiliaji," alisema Suluo.

Suluo alisema walibaini kwamba mchezo huo wa madereva kuchezea mfumo umekuwa ukifanywa kwa kushirikiana na kampuni ambazo zilipewa kazi ya kufunga vifaa hivyo ya U-track Afrika Ltd na Easy Track Solution JV, RJ Motchand Ltd ambayo nayo yamesimamishwa na LATRA.

Suluo alisema wameanza kuchukua hatua ya kudhibiti basi zinazobeba wanafunzi kutokana na kuendelea kuripotiwa matukio ya unyanyasaji kwa wanafunzi hao ambayo pia ni kinyume cha maadili.

"Kumekuwa na matukio ya kuwafanyia vitendo vya kikatili wanafunzi hasa wa kike kwenye basi za shule na zipo taarifa za wanafunzi hawa kunajisiwa, jambo hili halivumiliki na halikubaliki kwa ustaarabu wetu Watanzania," alisema Suluo.

Alitoa maelekezo kwa shule zote kuwasilisha orodha ya basi zinazotoa huduma kwa shule husika na majina ya madereva na



leseni zao, orodha ya wahudumu (matroni na patron) pamoja na namba zao za vitambulisho vya taifa.

Alisema, mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inafanya mapitio ya kanuni za usafiri wa umma ili kuongeza vigezo vya udhibiti wa basi hizo za shule.

Kadhalika, alisema mamlaka hiyo ilikumbusha wamiliki wa mabasi hayo kusimamia maadili kwa kuhakikisha hayaonyeshi, kupiga nyimbo au kuonyeshwa video zisizo na maadili wala kuwapo na watu wanaohubiri.

"Hili tulishalisema na tunarudia tena, kila mtoa huduma aanze kutathmini video na miziki inayopigwa kwenye gari yake, kwamba endapo akikaa na mwanawe, mzazi au mtu anayemheshimu, anaweza kuziangalia au kusikiliza?" alihoji Suluo.

"Kuhusu suala la kuwapo wanaohubiri kwenye basi, tulishalikataza na tunaendelea kusisitiza tena, hatutaki kuona mambo haya yanafanyika kwenye basi kwa sababu siyo mahali pake. Na katika hili tutachukua hatua kali kwa wale watakaobainika kukiuka," alisisitiza.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng`anzi, alisema kutokana na baadhi ya madereva kuchezea mfumo wa VTS, Jeshi la Polisi limeongeza mfumo mwingine wa udhibiti mwendo kwa madereva hao wawapo safarini ambao hautaruhusu gari lolote kutembea mwendo zaidi ya 80.

"Mfumo wa VTS utaangalia mwenendo wa uendeshaji wa gari na wa 'speed governor' utaangalia mwendo na gari na haitakwenda mwendo zaidi ya 80. Na tumeshaagiza tayari kwamba magari yote mapya yanayoingia nchini kuanzia Desemba, mwaka jana, yafungwe mfumo huo," alisema.




# Mil. 895/- zalambwa mikopo vikundi hewa

**Na Restuta James**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam imetajwa kinara wa kutoa mikopo ya Sh. 698,700,000 kwa vikundi hewa 34 wakati Manispaa ya Temeke ikitoa Sh. 178,536,140 kwa vikundi vya aina hiyo tisa.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere ya ukaguzi wa Serikali za Mitaa, iliyotolewa jijini Dodoma wiki iliyopita, inaonyesha kwamba Halmashauri ya Meru inafuatia kwa kutoa mikopo ya Sh. 18,700,000 kwa vikundi hewa.

"Nilishindwa kujiridhisha juu ya kuwepo kwa vikundi 48 vilivyopewa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 895.94 kwenye Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa. Aidha, nilibaini kuwa, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika hawakufahamu lolote kuhusu vikundi hivyo," ilieleza sehemu ya ripoti ya CAG.

Katika taarifa hiyo, CAG alishauri Ofisi ya Rais kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iwachukulie hatua waliotoa fedha kwa vikundi visivyokuwapo kwa kuwapeleka kwenye vyombo vya uchunguzi.

"Ninashauri Ofisi ya Rais TAMISEMI ichukue hatua stahiki kwa watumishi waliotoa mikopo kwa vikundi ambavyo hapakuwa na taarifa za kuwapo kwao ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye vyombo vya uchunguzi," alisema.

Wakati huo huo, CAG Kichere amebaini kuwa vikundi 19 katika Manispaa ya Temeke, vilikopa Sh. milioni 412.63 na kusitisha biashara.

Aidha, katika eneo hilo, Halmashauri ya Mji wa Geita inaongoza kwa kuwa na vikundi 396 vilivyokopa na vimeshasitisha biashara, ambavyo vinadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.05.

Wakati huo huo, Manispaa ya Temeke imebainika kutoa mikopo ya Sh. milioni 147.26 kwa vikundi vitano vilivyokuwa na wanachama wenye ajira rasmi, kinyume cha utaratibu.

"Tathmini yangu kuhusu mikopo iliyotolewa kwa vikundi nilibaini kuwa, mamlaka tisa za Serikali za Mitaa zilikuwa zikitoa mikopo ambayo haijarejeshwa yenye jumla ya Sh. bilioni 2.25 kutoka kwenye vikundi 627 vilivyositisha shughuli zao za biashara," ilieleza ripoti ya CAG.

Halmashauri zingine na kiasi cha fedha zilizotolewa ni Maswa (Sh. milioni 179.66), Wilaya ya Geita (Sh. milioni 176.52), Jiji la Arusha (Sh. milioni 141.32), Wilaya ya Tandaimba (Sh. milioni 121.54), Busega (Sh. milioni 32.92), Monduli (Sh. milioni 105.38) na Mji wa Mbulu (Sh. milioni 27.77).

HABARI KITAIFA

# Waliotajwa ripoti ya CAG wazidi kuwekwa kikaangoni

**Na Vitus Audax,** KWIMBA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali inaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wote waliotajwa kuhusika na ubadhirifu wa fedha za serikali katika ripoti iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Dk. Mpango alisema hayo jana katika kijiji cha Hungumalwa, Kwimba mkoani Mwanza wakati akisalimiana na wananchi katika ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Mwanza.

Alisema serikali haitawakalia kimya wote wanaobainika kuhusika na upotevu wa fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi. Alisema serikali itahakikisha kila mhusika anachukuliwa hatua za kisheria ili fedha za umma ziheshimiwe.

"Tayari hatua zimeanza kuchukuliwa kwa waliotajwa katika ripoti ya CAG na hatutaishia hapo. Tutaendelea kuchukua hatua kwa kila aliyetajwa na kubainika kuhusika katika ubadhirifu huu unaorudisha nyuma juhudi za serikali," alisema.

Dk.Mpango pia aliwaagiza viongozi wote mkoani Mwanza kuhakikisha wanafanyia kazi kesi zote zilizotajwa katika ripoti hiyo na kutatua yale yanayowezekana kufanyika ndani ya mkoa.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango alitembelea mradi wa kuzalisha mitambo bora ya ng'ombe katika shamba la Mabuki ulioko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mradi huo wa ng'ombe wa nyama unawanufaisha vijana 85 waliohitimu vyuo vya mifugo na kukosa ajira.

Mradi huo unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ukiwa na vituo atamizi nane. Katika eneo la Mabuki pekee, kuna ng'ombe 500 wanaoendelea kunenepeshwa kwa lengo la kuwauza kwa wafugaji ili kubadili sekta ya mifugo kutoka katika ufugaji wa mazoea na kuwa wenye tija kwa kuzalisha maziwa na nyama kwa wingi.

Akiwa katika mradi huo, Dk. Mpango aliagiza wizara kutuma wataalamu kwa wafugaji ili kuwaelimisha na hatimaye wafuge kwa tija na kuacha ufugaji wa kimazoea. Alisema serikali iko tayari kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika mradi huo na kutatua kero za waendeshaji wa mradi ili kuhakikisha unaleta tija kwa taifa.

Awali, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, alisema mradi huo ni sehemu ya mkakati wa serikali katika kuhakikisha wanaboresha sekta ya mifugo nchini ili kuleta tija kwa wafugaji wote na taifa kwa ujumla.

Pia alisema mikakati ya wizara hiyo ni pamoja na kuboresha mifugo nchini ili kutoa maziwa na nyama kwa wingi kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi huku akiwataka wafugaji kujitokeza kununua ng'ombe walionenepeshwa ili kuongeza uzalishaji katika sekta hiyo.

# Waliofutiwa matokeo kufanya tena mitihani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewapa fursa ya kurudia mtihani wa kidato cha nne kuanzia Mei 2, mwaka huu, watahiniwa 337 waliofutiwa matokeo kwa kufanya udanganyifu na kuandika matusi.

Aidha, imetoa onyo kwenye mitihani ya kidato ya sita itakayofanyika sambamba na inayorudiwa kuwa itakuwa macho kuangalia shule zitakazofanya udanganyifu.

Serikali pia imesema inaifanyia uchunguzi shule moja ambayo imekuwa ikitumia wanafunzi wa darasa la tano na sita kuwafanyia mitihani wanafunzi wa darasa la nne.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema wamejadiliana na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) ili kuona namna ya wanafunzi hao kufanya mtihani mapema kabla ya duru nyingine na suala hilo halitarudiwa tena.

"Nimeelekeza wanafunzi hao kama wakitaka wawasiliane na Baraza ili kufanya mtihani wa kidato cha nne na utatolewa wakati wa mtihani wa kidato cha sita ambao utaanza Mei 2 hadi 22, mwaka huu," alisema.

Alisema gharama za uendeshaji wa mtihani huo zitakuwa ndogo na kama ingeendeshwa nje ya utaratibu huo ingegharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni moja.

"Wasimamizi wa mitihani watakuwa wale wale wa kidato cha sita na watafanya kwa utaratibu utakaowekwa na utafungwa kwenda kusahihishwa.Hii ni mara ya mwisho kufanya hivi hatuwezi kuingiza nchi kwenye gharama hizi," alisema.

Aliwataka wazazi watambue kuwa suala la kushinikiza baada ya kufanyika udanganyifu halilipi.

Alibainisha kuwa shule zilizofanya udanganyifu ambazo ni Twibhoki, Thaqaafa, Mnemonic Academy ya Zanzibar na Cornel zitaendelea kuwa chini ya uangalizi na serikali haiwezi kukubali kusajili shule kwenda kuwa kiwanda cha kuharibu mfumo wa elimu.

"Uchunguzi ukikamilika tutatangaza uamuzi ambao Kamishna atafanya, mimi ningekuwa mzazi nisingepeleka mwanangu kwenye shule iliyopo chini ya uangalizi," alisema.

Awali, Prof.Mkenda alifafanua kuwa Novemba mwaka jana ilifanyika mitihani ya kidato cha nne na NECTA lilifuata matokeo ya watahiniwa 337.

Alisema watahiniwa 333 walifutiwa matokeo yao kwa ajili ya udanganyifu na wanafunzi wanne walifungiwa matokeo yao kwa sababu ya kuandika matusi kwenye karatasi za majibu.

"Kati ya wanafunzi 333 ambao matokeo yao yalizuiliwa wanafunzi 206 wanatoka katika shule mbili tu ambazo ni Twibhoki mkoani Mara na Thaqaafa jijini Mwanza, takribani mbili ya tatu ya wanafunzi wote waliozuiliwa matokeo wanatoka katika shule hizi mbili," alisema.

Alisema watahiniwa hao wanaweza kuomba kufanya mitihani kwenye duru ya mitihani inayofuata ya kidato cha nne kama watahiniwa binafsi.

Waziri huyo alisema wizi wa mitihani una madhara makubwa na kuwataka watanzania kukemea suala hilo na kuwa shupavu kupambana nalo.

"Wizi wa mitihani ni utovu wa maadili na moja ya maadili ni kutowafundisha watoto wetu wizi, wizi huu unaondoa weledi,"alisema.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.**

| | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | |
| a) Monthly | | FREE | | FREE |
| b) Interm | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | TZS | 12,800.00 | $ | 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | TZS | 12,800.00 | $ | 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | TZS | 5,100.00 | $ | 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges<br>a) Monthly | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| b) Interm | Fixed TZS | 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page TZS | 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | TZS | 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | |
| a) Inward | TZS | 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | |
| a) Inward | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | TZS | 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | |
| Upto 100,000 | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | TZS | 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | TZS | 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | TZS | 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | |
| Upto 100,000 | TZS | 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | TZS | 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | TZS | 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | TZS | 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | TZS | 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | |
| 1.SMALL | TZS | 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | TZS | 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | TZS | 635,600.00 | | NA |

| **E. REMITTANCES** | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | TZS | 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 | |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | TZS | 17,000.00 | $ | 9.00 |
| 1001 to 5000 | TZS | 20,400.00 | $ | 11.00 |
| 5001 to 10000 | TZS | 40,700.00 | $ | 22.00 |
| 10,001 and above | TZS | 84,800.00 | $ | 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 51.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 16.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 26.00 |
| **F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - TZS | 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | Upto 50,000 FREE | !"#$%& |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - TZS | 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - TZS | 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS TZS | 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | NA | | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | NA | | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | NA | | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | NA | | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | NA | | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | NA | | | $119.00 |
| Confirmation Commission | NA | | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | NA | | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | NA | | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | NA | | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Amendments | NA | | | $64.00 |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.25% | 2.50% | 3.25% |
| 181-364 days | 3.00% | 3.50% | 4.00% |
| Above 1 year | 3.50% | 4.00% | 4.25% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| RAHUL DIVECHA | ACTING HEAD BUSINESS OPERATIONS | SIGNED | 11-04-2023 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 11-04-2023 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 11-04-2023 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viwanda tanzu MSD vitapunguza matumizi fedha za kigeni

**KATIKA** mafanikio ambayo BOHARI ya Dawa (MSD) inajivunia ni kujenga viwanda vitakavyozalisha vifaa tiba nchini na kuipunguzia serikali mzigo wa kutumia fedha za kigeni kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi.

Wakati ugonjwa wa UVIKO-19 ulipoingia nchini kwa kasi miaka miwili iliyopita, Tanzania ilihitaji vifaa tiba kwa wingi ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo na kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji.

Siku zote panapojitokeza changamoto, ndipo watu hupata suluhisho la kupambana na kuja na jibu la kuondokana na changamoto hiyo.

Katika kupambana na changamoto ya kuagiza vifaa tiba kutoka nje, MSD imetaja hatua mbalimbali inazochukua ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda viwili vya barakoa na kimoja cha kuzalisha mipira ya mikono.

Idara ya Mipango, Tathmini na Ufuatiliaji ya MSD, imeeleza sababu za bohari hiyo kuanzisha kampuni tanzu na viwanda vyake.

Katika viwanda hivyo, kiwanda cha kutengeneza barakoa kimejengwa jijini Dar es Salaam, eneo la Keko, wilayani Temeke na uwekezaji wake ni Sh. bilioni 1.4.

"Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha barakoa 80 kwa dakika, uwekezaji wake ni Sh. bilioni 1.4 ambacho kwa mwaka kinazalisha barakoa milioni 5.8, kilianza kazi Agosti 2020. Kiwanda hiki kinaonesha umuhimu wa viwanda, kilianza kazi wakati wa janga la UVIKO-19 na wakati ule haikuwa rahisi kupata barakoa.

"Kabla ya kuanzisha kiwanda hiki, barakoa moja ilikuwa ikiuzwa Sh. 1,600, lakini kwa sasa inauzwa Sh. 500, na uwapo wa kiwanda hiki umesaidia Tanzania kuacha kuagiza nje ya nchi na hivyo kiwanda kimepunguza matumizi ya fedha za kigeni." MSD inafafanua

Kiwanda kingine cha kuzalisha barakoa ni cha N95 kilichozinduliwa rasmi Machi, mwaka huu, chenye uwezo wa kuzalisha barakoa 100 hadi 150 kwa saa moja.

Kuhusu kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono, kilichopo Idofi mkoani Njombe, kinatarajia kuanza uzalishaji Julai, mwaka huu na kitakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji kwa asilimia 100.

"Kiwanda kitatoa ajira zaidi ya 200 za moja kwa moja na ambazo sio za moja kwa moja. Viwanda vyote hivyo vitaokoa fedha za kigeni na tunataka malighafi za viwanda hivi zitoke nchini. Tukifanikwa tutatengeneza mzunguko mzuri wa fedha na kuimarisha uchumi."


Hatua hii ya MSD sio tu inaokoa fedha za kigeni, bali pia inasaidia kupunguza tatizo la ajira linaloikabili nchi kutokana na vijana wengi kukosa ajira wamalizapo vyuo.

Viwanda hivyo vitasaidia kutoa ajira za kudumu na zisizo za kudumu na kupunguza tatizo la vijana wanaozagaa mitaani kutafuta ajira.

Vile vile, viwanda hivyo vitasaidia wakulima wa hapa nchini kwa sababu vitahitaji malighafi inayozalishwa hapa hapa na kuwakomboa kwa kipato.

Kwetu sisi tunasema hatua hii ni kubwa na muhimu, kwa kuwa hapo mwanzo barakao zilikuwa zikiagizwa kutoka nje na kuuzwa kwa bei kubwa tofauti na zitakazozalishwa nchini ambazo zitakuwa na gharama nafuu na kila mtu atamudu kununua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kutoka wingi huu wa mimba zao wanafunzi, tuanze vita kukabili

**MIMBA** kwa wanafunzi zimeendelea kuwa tatizo sugu nchini kwa kipindi kirefu, licha ya jitihada mbalimbali za serikali na wadau wa elimu, katika kushughulikia ili kuhakikisha watoto wa kike wanatimiza ndoto zao za elimu.

Kimsingi, serikali imekuwa ikifanya jitihada kwa lengo la kutokomeza mimba hizo na kuwanusuru watoto wa kike walioko katika hatari ya mimba za utotoni ambazo mwisho wake si salama kwao.

Licha ya tatizo hilo kugusa hisia za kila mpenda maendeleo ya elimu, bado inaonekana kwamba jamii haijahamasika kutoa ushirikiano wa karibu kwa vyombo vya dola, ili kuwafichua wahusika wa vitendo hivyo.

Baadhi ya wazazi na walezi hutuhumiwa kupokea rushwa kutoka kwa watuhumiwa ili wasifikishwe kwenye vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua stahiki iwe fundisho kwao na kwa wengine wenye tabia za aina hiyo.

Inawezekana tuhuma hizo zikawa na ukweli ndani yake, kwani kuendelea kuwapo kwa mimba nyingi za wanafunzi, huku idadi ya watuhumiwa ikiwa hailingani na idadi ya waliopata mimba si sawa.

Inasikitisha kusikia kwamba ndani ya mwaka mmoja, katika kipindi cha kati ya mwaka 2021 hadi 2022, wanafunzi 9,011 wa shule za msingi na sekondari wamepata mimba. Hali inayoonyesha tatizo bado ni kubwa.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga ndiye anayebainisha hayo hivi karibuni, jijini Dodoma na kufafanua kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 na 2022 wanafunzi wa shule za msingi waliopata ujauzito ni 1,554 na sekondari ni 7,457.

Mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini, zinachangia kurudisha nyuma maendeleo yao kielimu, hivyo ni wazi ipo haja kwa wadau wote wa elimu kuendelea kushirikiana na serikali katika vita hii.

Ni vyema wazazi na walezi kushirikiana na vyombo vya dola kuhakikisha watuhumiwa wanakamatwa, ili sheria iweze kuchukua mkondo, kwani njia hiyo inaweza kupunguza wingi wa mimba hizo kama si kumaliza tatizo kabisa.

Kama jamii ingekuwa jambo jema kama itaona umuhimu huu, kwani Tanzania yenye wasomi wengi wa kike waliobobea katika fani mbalimbali itawezekana na maendeleo inawezekana iwapo watalindwa.

Lakini, kama jamii itaendelea kuwaficha wahusika wa vitendo hivyo, itakuwa ni sawa na kurudisha nyuma juhudi za serikali na wadau wa elimu za kuhakikisha mtoto wa kike anapata elimu bora.

Pamoja na hayo, ninadhani ipo haja kwa wanafunzi kupewa elimu ya kujitambua na kufahamu wajibu wao kwa jamii na taifa, ili wajithamini na kuepuka vishawishi vinavyosababisha wapate mimba au kuacha shule.

Kumekuwapo sababu nyingi ambazo zimekuwa zikitajwa kuchangia kuwapo kwa mimba, mojawapo ikiwa ni wazazi na walezi kuwa na tamaa ya kutaka kupata mali.

Sababu nyingine ni ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi, umbali wa shule na hasa sekondari za kata, ambazo husababisha wanafunzi kutembea kwa muda mrefu kufuata elimu na kujikuta wakikumbana na vishawishi njiani.

Hizo ni baadhi ya sababu zinazoendelea kutajwa huku kukiwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo ambalo linatakiwa kumalizwa ili watoto wa kike wawe huru.

Lakini ninaamini kuwa wanafunzi wa kike wakipewa elimu ya kujitambua na kufahamu wajibu wao kwa jamii na taifa, hawatakuwa tayari kukubaliana na uamuzi wa wao au kukubali vishawishi vya njiani.

Kwa ujumla ni kwamba, mimba bado zimeendelea kuwapo na sababu za mimba hizo ni zile zile, ambazo inawezekana bado huenda sasa zinatakiwa zifanyiwe kazi ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

Njia mojawapo ya ufumbuzi wa kudumu ni kuwapo elimu ya kujitambua ili wasishawishike kirahisi na kujikuta wakipata mimba na kukatisha masomo au kukataa shule na kuingia katika ndoa za utotoni.

TANGAZO

International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA | MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2022 | 31.12.2021 |
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,449 | 993 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 7,225 | 12,357 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 19,106 | 18,471 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 976 | 3,425 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (11) | 2 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 17,993 | 22,098 |
| 12 | Mali Nyingine | 15,480 | 16,311 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 358 | 417 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **62,576** | **74,074** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 32,772 | 44,380 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 162 | 162 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | 3 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 682 | 982 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 61 | 61.15 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,653 | 2,932 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | ***JUMLA YA DHIMA*** | **36,331** | **48,520** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **26,245** | **25,554** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,937 | 28,937 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,747 | 2,254 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (17,595) | (6,453) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 304 | (11,035) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,851 | 11,851 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **26,245** | **25,554** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 477 | 617 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 7,718 | 6,450 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,926 | 1,390 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 41.94% | 34.50% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 35.49% | 26.43% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 66.03% | 54.79% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 28.75% | 29.83% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 60.85% | 59.39% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -26.06% | 18.67% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -15.52% | 10.47% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2022 | 31.12.2021 |
| 1 | Mapato ya Riba | 5,080 | 4,542 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,839 | 1,854 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***3,241*** | ***2,688*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 11,404 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 494 | 1,630 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **3,498** | **498** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 88 | (13) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 52 | 100 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 3,358 | 412 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **5,444** | **5,401** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,970 | 2,095 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 92 | 449 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 3,382 | 2,857 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **802** | **(15,249)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (497) | 4,214 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **304** | **(11,035)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **304** | **(11,035)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 55 | 58 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 15 | (551) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | 15 | (551) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | 0.45% | -15.64% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.18% | -43.59% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 63.46% | 107.16% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 7.90% | 5.67% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA | MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2022 | 31.12.2021 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 802 | (15,249) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 883 | 1,891 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,516 | 12,004 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (12,021) | 6,902 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 70 | (379) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 5,483 | (2,327) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (22) | (49) |
| | -SMR | 309 | (45) |
| | - Mengineyo | | |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(981)*** | ***2,749*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (5,473) | (165) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (372) | (8,989) |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(5,845)** | **(9,154)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 11,851 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **-** | **11,851** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(6,826)** | **5,446** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 14,355 | 8,909 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **7,529** | **14,355** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **28,937** | **11,851** | **(17,488)** | **2,254** | **25,554** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | 386 | - | 386 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | 304 | | 304 |
| | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (493) | 493 | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | |
| Mengineyo | | | | | |
| | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | | | | | - |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2022** | **28,937** | **11,851** | **(17,291)** | **2,747** | **26,245** |
| | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **28,937** | **-** | **(11,316)** | **7,455** | **25,075** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (337) | - | (337) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (11,035) | | (11,035) |
| | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | - |
| Ziada ya Kisheria | | | 5,201 | (5,201) | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | |
| Mengineyo | | | | | |
| | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | | 11,851 | | | 11,851 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2021** | **28,937** | **11,851** | **(17,488)** | **2,254** | **25,554** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zilikaguliwa na Nexia SJ "Certified Public Accountant" na kupata hati safi

Taarifa hii ya fedha ilihidhiniswa na Bodi ya Wakurugenzi Tarehe 29 Machi 2023 na kusainiwa na:-

**Bw. Thomas Eustace Rwebangira**

**Bw. Alfred L Mkombo**

# 77 mbaroni, sita watuhumiwa mauaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linawashikilia watu 77 kwa makosa mbalimbali huku sita kati yao wakituhumiwa kwa makosa ya mauaji ya mlinzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, akizungumza na waandishi wa habari juzi alisema tukio hilo lilitokea Machi 28, mwaka huu, usiku eneo la Lulanzi, Picha ya Ndege kwa watu wanaodhaniwa majambazi kuvamia duka la Paulo Mlay kisha kumuua mlinzi, Alex Patakiri (25).

Kamanda Lutumo alisema watu hao walipovamia duka hilo waliiba vitu na kufanya mauaji hayo.

Alisema baada ya tukio hilo polisi ilifanya msako na taarifa za kiintelejensia pamoja na ushirikiano wa raia wema watuhumiwa walikamatwa wakiwa na vitu walivyoiba.

Alisema watuhumiwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo baada ya upelelezi kukamilika.

Kamanda Lutumo alisema kuwa katika mapambano ya dawa za kulevya, Polisi walikamata mihadarati (bhangi) puli 48 na kete 382, dawa za kulevya heroin kete 14, pombe ya moshi lita 93.

Aidha, katika kupambana na magendo mwambao wa bahari Jeshi hilo lilikamata mafuta ya kula dumu 166 yaliyoingizwa nchini kwa kukwepa kodi.

Katika hatua nyingine, Jeshi hilo limewaita walioibiwa pikipiki kufika kituo cha Polisi Mji kilichopo Kibaha kuzitambua pikipiki zao ambazo zimekamatwa zikidhaniwa ni za wizi.

Alitaja aina ya pilipiki hizo kuwa ni MC 585 DGP aina ya TVS nyeusi, MC 908 DAK Boxer nyeusi na MC 538 DOR aina ya Haujue nyeusi.



Vijana wakijiajiri kwa kuvusha watu kwa ujira wa 10,000/- baada ya daraja kubomolewa na mvua kubwa iliyonyesha na kukata mawasiliano katika kata za Ubagwe, Ulewe na Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Watu 30 waomba kujenga vituo vya mafuta

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imesema watu 30 wameomba leseni ya kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta na petroli.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana na Mkurugenzi, Dk. James Andilile, Sheria ya Mafuta Na 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu Mamlaka hiyo kusimamia shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

Alisema kifungu cha 13 (1) cha sheria kinawataka wote wanao jihusisha na sekta hizo kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kwenye tangazo hilo, pia alisema mtu yeyote au kikundi cha watu watakapo kutana na pingamizi la kutopewa leseni watoe taarifa EWURA, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo kupitia anwani yao.

**Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana na Mkurugenzi, Dk. James Andilile, Sheria ya Mafuta Na 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu Mamlaka hiyo kusimamia shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.**

# MSD yajivunia kuondoa uagizaji vifaa tiba nje

**Na Elizabeth Zaya**

BOHARI ya Dawa (MSD) imetaja hatua mbalimbali inazochukua kuondokana na changamoto ya kuagiza vifaa tiba kutoka nje, ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda viwili vya barakoa na kimoja cha kuzalisha mipira ya mikono.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Hassan Ibrahimu kutoka Idara ya Mipango, Tathmini na Ufuatiliaji wa MSD, alipokuwa akielezea sababu za bohari hiyo kuanzisha kampuni tanzu na viwanda vyake wakati akizungumza kwenye semina ya wahariri wa vyombo vya habari iliyoandaliwa na MSD, jijini Dodoma.

Alisema moja ya kiwanda cha kutengeneza barakoa kipo Dar es Salaam, eneo la Keko, wilayani Temeke na uwekezaji wake ni Sh. bilioni 1.4.

"Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha barakoa 80 kwa dakika, uwekezaji wake ni Sh. bilioni 1.4 ambacho kwa mwaka kinazalisha barakoa milioni 5.8, kilianza kazi Agosti 2020. Kiwanda hiki kinaonesha umuhimu wa viwanda, kilianza kazi wakati wa janga la UVIKO-19 na wakati ule haikuwa rahisi kupata barakoa.

"Kabla ya kuanzisha kiwanda hiki, barakoa moja ilikuwa ikiuzwa Sh. 1,600 lakini kwa sasa inauzwa Sh. 500, na uwapo wa kiwanda hiki umesaidia tuache kuagiza nje ya nchi, kwa maana hiyo kiwanda kimepunguza matumizi ya fedha za kigeni," alisema Ibrahim.

Pia, alisema kiwanda kingine cha kuzalisha barakoa ni cha N95 kilichozinduliwa rasmi Machi, mwaka huu, chenye uwezo wa kuzalisha barakoa 100 hadi 150 kwa saa moja.

Kuhusu kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono, kilichopo Idofi mkoani Njombe, alisema kinatarajia kuanza uzalishaji Julai, mwaka huu na kitakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji kwa asilimia 100.

"Kiwanda kitatoa ajira zaidi ya 200 za moja kwa moja na ambazo sio za moja kwa moja. Viwanda vyote hivyo vitaokoa fedha za kigeni na tunataka malighafi za viwanda hivi zitoke nchini. Tukifanikwa tutatengeneza mzunguko mzuri wa fedha na kuimarisha uchumi," alisema Ibrahim.





# Mvua yaharibu mawasiliano ya barabara

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa vitongoji cha Njia Panda Mashariki, Faru na Darajani katika mji mdogo wa Himo, Moshi mkoani Kilimanjaro, wanakabiliwa na ukosefu wa mawasiliano ya barabara ya kuingia na kutoka baada ya barabara ya Elimo waliyokuwa wakiitumia kuharibiwa na mvua.

Kutokana na hali hiyo, mmoja wa wananchi hao, Yolanda Kimario, amesema kipindi hiki cha mvua wamekuwa wakilazimika kuwazuia watoto kwenda shuleni kutokana na kuhofia maji ya mvua yanayotiririka kwa wingi katika makorongo yaliyoko kitongojini hapo.

Alisema kwa sasa usalama wa watoto ni mdogo wanapokwenda shuleni hali ambayo imekuwa ikiwalazimu baadhi ya wazazi kuhakikisha wanawapeleka na kuwarudisha nyumbani.

Yetonsia Kiring'a alisema kwa sasa wajawazito wamelazimika kujifungulia nyumbani kutokana na magari kushindwa kufika kuwachukua na kuwapeleka hospitalini hali ambayo imekuwa ikihatarisha maisha ya mtoto na mama.

"Wapo ndugu zetu wagonjwa tumeshindwa kuwafikisha hospitalini kutonana na kukosa barabara na wakati mwingine inapobidi tumekuwa tukiwabeba mgongoni na kwenye machela kuwatoa barabara kuu ili kupata huduma ya usafiri. Tunaiomba sana serikali ituangalie kwa jicho la kipekee," alisema.

James Maleko, mkazi wa Kitongoji cha Njia Panda Mashariki, alisema kwa sasa wameshindwa kufanya shughuli za maendeleo kutokana na barabara kuu ya kuingia na kutoka katika kitongoji hicho kuwa mbaya na magari kushindwa kupita. Alisema hali hiyo imewalazimu kulaza magari yao katika vituo vya mafuta Njia Panda na Himo.

Maleko aliiomba serikali kufanya juhudi za haraka kurejesha mawasiliano ya barabara ya Elimo ili kuwaondoa wananchi wa vitongoji vya Faru, Njia Panda Mashariki na Darajani ambao kwa sasa ni sawa na wapo katika kisiwa.

Akizungumzia kuhusu kero hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Mji Mdogo wa Himo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Darajani, Richard Njau, alisekuwa wananchi wana haki ya kulalamika kutokana na kuitegemea barabara ya Elimo kuingia na kutoka ambayo kwa sasa haipitiki baada ya kusombwa na maji.

Njau alisema kutokana na uharibufu uliotokana na mvua kusababisha watoto kushindwa kwenda shuleni na hata wajawazito kushindwa kwenda kliniki na hata wakati mwingine hospitali kujifungua pindi wanapofikia.

Mwenyekiti wa Shina Namba Nbili kitongoji cha Njia Panda Mashariki, Faustine Abel, alisema ameshachukua hatua za haraka za kumshirikisha Diwani wa Njia panda, Loveness Mfinanga, kuhusu kuharibika kwa barabara hiyo ambayo diwani huyo alimwahidi kulifikisha tatizo hilo TARURA.

## Wauguzi wafundishwa kupima usikivu watoto

**Na Oscar Assenga,** TANGA.

WAUGUZI katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, wamefundishwa namna ya kupima usikivu wa watoto wadogo wanapozaliwa ili kutoa huduma hiyo kwa ufanisi na tija.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo mwishoni mwa wiki, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Edwin Liyombo, alisema wameamua kuwafundisha wauguzi programu ya kupima usikivu kwa watoto wanaozaliwa ili kuwasaidia wanapokuwa na shida hiyo pindi wanapozaliwa.

Dk. Liyombo alisema imebainika kuna watoto wengi wanajulikana wana matatizo ya usikivu na wanashindwa kuongea pindi wanapokuwa na umri wa kuanza kwenda shuleni ikiwamo wanaozaliwa hawawezi kuongea, hivyo mpango huo unasaidia kugundua mtoto pale anazaliwa mpaka mwezi mmoja.

Alisema kwa sababu kuna mashine maalumu ya kuwapima kama wana matatizo na wakibainika mapema inawasaidia kuona namna ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

"Tunawafundisha wauguzi jinsi ya kufanya uchunguzi na baadaye itakwenda nchi nzima kwani hawa wanaowafundisha baadaye watakuwa walimu na kufundisha wengine lakini tutawaletea mashine ndogo itakayotumika kupima watoto wanapozaliwa," alisema.

Dk. Liyombo aliwaomba watu wajitokeze wakati wa mpango huo wa kupima usikivu huku akibainisha kuwa wamepima watoto 20 na wengi hawana matatizo lakini kadiri watakavyopima wengi watajua hali iko vuzri, hivyo kuisaidia wizara kupanga bajeti kuona namna ya kuwasaidia.

Katika hatua nyingine, Dk. Liyombo alisema takwimu zinaonyesha kwamba kati ya watu 100, saba wana tatizo la usikivu wakiwamo watoto wadogo ndiyo maana Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilianzisha program ya kuweka kipandikizi kwa ajili ya kusikia na mpaka sasa watoto 57 wamefanyiwa tangu mwaka 2017.

Alisema watoto wengi wanakuwa na matatizo wakati wanazaliwa au wakiwa na umri mdogo, hivyo wameona wakiwagundua mapema itasaidia kufuatilia kuona ni sababu zipi zinafanya kuwapo kwa hali hiyo.



Mchuuzi Mwanaisha Ally (kushoto), akimuuzia boga mteja kwenye eneo la Masjid Noor katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. Maboga ni moja ya chakula kinachopendwa kwa maandalizi ya futari hasa wakati wa mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan. Boga moja liliuzwa kwa bei ya 1,000/- hadi 3,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: GIFT THADEY**

# Walimu waonywa kuhusu mikopo umiza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WALIMU wameonywa kuacha kukopa kwenye taasisi za kifedha ambazo zinawaumiza kwa kulipa riba kubwa na kuwasababishia majuto baada ya mikopo hiyo.

Ofisa Ushirika wa Jiji la Arusha, Omary Mrugeni, aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akifungua warsha ya kuwajengea uwezo wanachama wa Chama cha Kuweka na Kukopa (SACCOS) cha Walimu wa jiji hilo, Arusha Teachers SACCOS.

"Tafadhali kopeni kwenye vyama vyenu au taasisi zilizosajiliwa kisheria. Epukeni kwenda kukopa kwa matapeli wanaowaletea majanga na majuto baadaye," alisema.

Aidha, alisema kuna manufaa makubwa mwalimu anapokopa katika chama chake kwa kuwa husaidia kuimarisha ushirika na kuviongezea nguvu zaidi ya kifedha.


Kadhalika, aliwaagiza viongozi na watendaji, kuhakikisha kuwa wanaendesha vyama vyao, kwa kufuata taratibu kanuni na misingi ya ushirika.

Mwenyekiti wa Arusha Teachers SACCOS, Ahamonhery Zelote, alisema lengo la warsha hiyo ni kutoa elimu kwa wanachama ili wajuwe umuhimu wa ushirika,wajibu na haki zao katika chama.

"Nawaomba walimu wa jiji hili wajiungie kwenye SACCOS kwani kwa jiji hili tuna zaidi ya walimu 2,000 lakini wanachama wako 472 tu. Naomba tuhamasishane ili wote wajiunge huku," alisema.

Naye Meneja wa Chama hicho, Edna Laizer, alishangazwa na baadhi ya wanachama kukimbilia kukopa katika benki na taasisi zingine za kifedha na kupoteza muda mwingi kufuatilia mikopo, huku wakitozwa riba kubwa tofauti na chama chao.

Katika warsha hiyo, mada mbili ziliwasilishwa ambazo ni haki na wajibu wa mwanachama, pamoja na kujenga na kukuza mtaji wa chama, huku baadhi ya washiriki Abdul Mmbaga na Samwel Mkhandi wakipongeza kupatiwa mafunzo yaliyokuja wakati mwafaka.



# Serikali yadhamiria kunusuru ufugaji

**Na Vitus Audax** MWANZA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeonyesha dhamira yake ya kuinua sekta ya mifugo na ufugaji nchini kwa kuwekeza katika ufugaji wa kisasa ambao utazalisha mifugo yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha maziwa na nyama na kuuzwa kwa wafugaji kwa bei yenye ruzuku.

Lengo la serikali ni kuzalisha ng'ombe bora watakaosaidia kuondoa zao la ng'ombe ambalo linatumiwa na wafugaji nchini bila kuwa na faida huku katika mpango huo tayari serikali imeweka ng'ombe 500 katika kituo cha Mabuki wanaoendeshwa chini ya usimamizi wa vijana waliowezeshwa na serikali kuinua zao hilo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, alipokuwa akizungumza kutokana na ziara ya Makamu wa Rais, Dk. Philp Mpango mkoani Mwanza.

Alisema serikali inakusudia kuimarisha sekta hiyo kwa kutumia vituo atamizi vinane vilivyoko maeneo mbalimbali nchini ili kuwasaidia wafugaji kuondokana na matatizo wanayokumbana nayo kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Ulega alisema serikali imetenga mashamba nane yatakayosaidia kuwafundisha wafugaji kufuga kibiashara ili kusaidia upatikanaji wa mifugo bora itakayosaidia pia kupatikana kwa nyama inayofaa kuuzwa katika masoko ya kimataifa.

Kadhalika alisema serikali inaimarisha mashamba ya malisho pamoja na usambazaji wa teknolojia katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya bara la Afrika ili kuzisaidia nchi nyingine katika kukuza sekta ya mifugo.

"Kwa mkoa wa Mwanza tayari tumeweka mabanda yenye thamani ya Sh. milioni 32 kwa ajili ya kufugia ng'ombe hao wa kisasa. Kila banda lina uwezo wa kuhifadhi ng'ombe wa kunenepeshwa 100. Lengo letu ni wafugaji wote wawe na ng'ombe wanaokidhi vigezo vya soko la ushindani," alisema Ulega.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema serikali mkoani humo ipo tayari kuhakikisha sekta ya mifugo inaendelea kuwanufaisha Watanzania na vijana kwa ujumla kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliopo mkoani hapa.

"Si kwa sekta ya mifugo kwa ufugaji wa ng'ombe pekee bali hata katika sekta ya ufugaji wa samaki tumeweka mikakati na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) ili kutoa vijana watakaofanya utafiti wa namna bora ya kufuga samaki kwa tija," alisema Malima.




Meneja Mkuu wa mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko (kulia) akisalimiana na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, wakati mgodi huo kwa kushirikiana na makandarasi wake, ulipokabidhi msaada wa vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Sungusungu, Nyamongo, wilayani Tarime, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watoto kuondolewa machimbo dhahabu

**Na Marco Maduhu,** GEITA

UONGOZI wa machimbo madogo ya madini ya dhahabu ya Nyamatagata yaliyoko Manga kata ya Mgusu Halmashauri ya Geita Mji, umedhamiria kuondoa watoto wote kutoishi ndani ya machimbo hayo kwa lengo la kulinda usalama wa maisha yao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Manga, Elias Lukanya, alisema juzi kuwa wamefikia hatua hiyo ikiwa ni sehemu ya kuwalinda watoto wadogo ili kuwaepusha na hatari ya kupoteza maisha wawapo katika maeneo hayo.

Alisema licha ya watoto wengine kuwapo mgodini hapo pamoja na wazazi au walezi wao waliopo humo kwa ajili ya kujipatia riziki, bado hatua hiyo ni hatari kwa maisha yao kwani bado wanategemewa na taifa huku wakikosa na haki zao zingine za kimsingi.

"Watoto kuishi kwenye machimbo haya ni hatari. Tayari tulishapoteza mtoto mmoja mwaka jana ambaye alitumbukia kwenye shimo ambalo linachimbwa dhahabu akafariki dunia," alisema Lukanya.

Mtendaji wa Kata ya Mgusu, Elias Galila, alisema watoto kuendelea kuishi kwenye machimbo hayo hawatapata pia fursa ya kusoma na kutimiza ndoto zao, hali ambayo taifa itazalisha watu wasiokuwa na elimu na hata kukosa wataalamu wakiwamo madaktari.

Kamanda wa Jeshi la Jadi Sungusungu kwenye machimbo hayo Mathias Mwita, alisema kwa sasa kazi ambayo wanaifanya ni kuorodhesha majina ya watoto ili kupata idadi kamili. Baada ya hapo, alisema watawaamuru wazazi wao kuwatoa eneo hilo na kubaki watu wazima tu na kazi hiyo itakuwa endelevu.

Mmoja wa wazazi hao, Judith Daudi, alisema wanakubali watoto kuondolewa kwenye machimbo hayo kwa sababu maisha yao yako hatarini kwa kutumbukia kwenye mashimo ya madini na pia wanakosa haki ya kupata elimu wawapo katika machimbo hayo.

# Auawa akidaiwa kutembea na mke wa mtu

**Na Mwandishi Wetu,** CHATO

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Mwabazengi Kata ya Muungano wilayani Chato mkoani Geita, Robert Msodoki, amepigwa hadi kufa baada ya kufumaniwa na mke wa mtu aliyejulikana kwa jina la John Mbonge, wakienda katika nyumba ya kulala wageni kutekeleza azma yao.

Tukio hilo lilitokea Aprili 9, mwaka huu, wakati wa sikukuu ya Pasaka na kwamba wawili hao walipofumaniwa wakielekea nyumba ya kulala wageni katika Kijiji cha Itale. Mume wa mwanamke huyo anadaiwa kuwa alikuwa akifuatilia nyendo zao tangu mwaka 2018 na amewahi kuwafumania mara mbili kabla ya kufikwa na umauti.

Akisimulia tukio hilo, Katibu wa Ulinzi Shirikishi, maarufu kama Sungusungu, katika kijiji cha Itale, Enos Joseph, alisema baada ya kupokea taarifa za fumanizi aliamua kwenda eneo la tukio pamoja na viongozi wenzake na kukuta tayari amepigwa na yuko katika hali mbaya na kumtambua huku akizungumza kwa shida.

"Nilimuuliza unanitambua akajibu kwa shida kuwa ndio wewe si ni Enos? Nikamuuliza imekuwaje ndipo akanijibu kuwa wake za watu wameniletea matatizo huku akimtaja John kuwa ndiye aliyemkata mapanga na kuchukua simu yake na baada ya maneno yale hakuongea tena," alisema.

Joseph aliongeza kuwa baada ya kuona mwenyekiti huyo ana hali mbaya, waliamua kumpeleka Hospitali ya Wilaya ya Chato kwa matibabu zaidi na baada ya kupimwa na muuguzi aliyempokea aliwaeleza kuwa tayari amefariki dunia.

Kutokana na tukio hilo, Joseph alisema tukio hilo ni la tatu huku matukio mengine ambayo alikuwa akifumaniwa alikuwa akilazimika kulipa faini na kusamehewa lakini hakuacha mpaka anafikwa na mauti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, ACP Safia Jongo, alisema mwenyekiti huyo alijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili wake baada ya kukutwa akiwa amesimama na mke wa mtu, huku akisema hajapewa taarifa za kifo chake.

"Nilipewa taarifa za mwenyekiti huyo kujeruhiwa vibaya upande wa paja la kulia, mkono na kichwani kutokana na wivu wa mapenzi na kwamba hali yake ilikuwa mbaya. Taarifa za kuwa ameshafariki (dunia) hizo nilikuwa bado sijatumiwa," alisema Jongo.

Kamanda Jongo alisema mtuhumiwa anayedaiwa kumjeruhi na kumsababishia mauti mwenyekiti huyo alikimbia kusikojulikana baada ya kutenda kosa hilo na jeshi hilo linaendelea na msako mkali wa kumtafuta ili sheria ichukue mkondo wake.



Ukurasa 12

**Mchangia uhuru aliyekimbia nchini miaka michache baada kuwa waziri**



Ukurasa 13

Miaka 39 bila ya Sokoine, ujasiri na uchapakazi wake ukibaki kuwa alama


# siasa

JUMATANO APRILI 12, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 13

**Wadau watoa ya moyoni, mahakama kukataa 'wagombea bila kupingwa'**

# Rais alivyotumia Ripoti CAG kuthibitisha kukubalika, uwazi, uwajibikaji kwa umma

• Kilichoamuliwa TRC yawa darasa aina yake

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea Taarifa ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 2021/22 kutoka kwa CAG Charles Kichere, Ikulu Jijini Dar es salaam, Machi Mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

NI ngumu sana kwa wataalamu wa siasa wanaeleza katika namna ya kutenganisha siasa na mwenendo wa uchumi na mara zote huwa zinategemeana. Siasa mara zote huamua jambo, huku uchumi ukiwa unaendesha hali halisi na maisha ya kila siku.

Wanasiasa hushikilia nyendo hizo, nguvu kuu ikiegemea penye undani wa uchumi. Nchini hadi sasa, kuanzia maisha ya kijamii na hata kisiasa, mada inayotawala kwa kiasi kikubwa ni Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22 , iliyotolewa siku chache zilizopita. Ni suala la fedha na uchumi, ikikamata nguzo ya kisiasa nchini.

Mara tu baada ya ripoti hiyo ambayo akamwasilishia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye naye anatolea ufafanuzi wa majibu na uamuzi, pasipo 'kuyakopa' bali akayafafanua kwa kina undani wake na mwelekeo wa kiserikali.

Dk. Samia akaeleza papo kwa hapo penye kasoro, akinena kwa tafsiri yenye kubainisha maeneo ambayo walakini ukitajwa. Pia, ni aina ya maelezo ambayo yanabeba sura ya kina katika mustakabali mkuu, umma ukishuhudia msimamo wa kirais kwa umma; uwajibikaji, uwazi, pia lugha na matendo ya kukubalika kwa umma.

Suala la uwazi unaanzia pale, CAG safari hii na hata mwaka uliopita awasilisha hilo katika mustakabali huo faragha kwa umma, kupitia vyombo hai vya habari ni maslahi ya umma na wanapaswa kujua.



Lakini katika hatua hiyo ya kwanza, nayo ikabeba sura nyingine ya pili ni pale Rais Dk. Samia akionyesha namna ya kuwajikibika, kuanzia taarifa ya awali pale Rais alipoonyesha baadhi ya maeneo kutokukubaliana na 'uchafu'; ulioanikwa na CAG na Rais Dk. Samia akiungana naye kukiri kuna uchafu.'

Ni mara moja, ripoti mpya ya CAG inaibua uwakibikaji unaochukua nafasi, ikirejewa katika uamuzi wa rais wikiendi iliyopita kuvunja Bodi ya Wakurugenzi na uongozi wa juu, akiungana na hoja ya CAO katika shirika hilo.

Kwa mujibu wa CAG, kuzidishwa muda wa mikakati ya mradi wa reli ya kisasa (SGE) unaendelea sasa, umekuwa na atahari ya kwanzs ni gharama kubwa, ukiwa umezidi kwa miaka kadhaa.

Vyama vya siasa kama kawaida yao havikukaa kimya, navyo vikaanza mara moja kuitoa michango yao kuhusu hoja na tukio hilo. Vilevile wadau nje ya vyama, wanaojumuisha wasomi na taasisi binafsi, vyote kwa pamoja vimekubaliana na hatua ya Rais Dk. Samia kwamba amekubalika.

Msingi wake huo pekee ni kwamba, ukaonekana kuwa hatua mbele ya Rais lakini ikavuka na kikubwa ambacho kinatokana na mchango wa umma wote tajwa, unaendelea hadi sasa, mfano ni baadhi ya wadau wakitaka kuwapo hatua zaidi, kulingana na hatua tajwa na CAG. Tayari vyama kama ACT Wazalendo na Chadema, vimeshanena yao, hali kadhalika taasisi binafsi.

Ujumla wake, unaibua mwelekeo bora katika taarifa hizo za CAG, ambazo zinaunda hata utamaduni na mwenendo sahihi katika dhana nzima ya sayansi ya uchumi, katika mustakabali mpana kama uwajibikaji, uwazi na kukubalika.

# Wadau watoa ya moyoni, mahakama kukataa 'wagombea bila kupingwa'



Thomas Ngawaiya (kushoto), katika moja ya mikutano ya CCM.

**Na Sabato Kasika**

KWA muda mrefu, katika siasa za Tanzania kumekuwapo na wagombea wanaopita bila kupingwa, kitendo ambacho kimekuwa kikilalamikiwa na baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani.

Hata hivyo, hivi karibuni Mahakama Kuu Masijala Kuu, Dar es Salaam, ilibadilisha vifungu vya sheria vinavyoruhusu kuwapo kwa wagombea wa aina hiyo ili kila anayewania uongozi, apande jukwaani kunadi sera kwa wananchi.

Kutokana na uamuzi huo, Nipashe imezungumza na baadhi ya wadau wa siasa ili kupata mtazamo wao kuhusu kile kilichofanywa na mahakama. Miongoni mwao ni mwanasiasa mkongwe Thoms Ngawaiya.

Huyo ni kada wa CCM, ambaye awali alishadumu katika ngome ya upinzani ikiwamo Chama Cha Tanzania Labour (TLP) chini ya Mwenyekiti, marehemu Agustino Mrema, sasa anapongeza uamuzi wa mahakama, kwa hoja kwamba unakwenda sawa na kile ambacho Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akikifanya cha kuimarisha demokrasia.

Ngawaiya ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA) anasema mahakama haina budi kupongezwa kwa uamuzi huo.

Anasema kulikuwapo na mchezo mchafu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi wa kubeba baadhi ya wagombea kwa kukataa kupokea fomu za wengine, ili wanaowataka wapite kirahisi.

"Bila kujali itikadi za vyama vyetu, tuipe mahakama hongera kwa uamuzi huo wa busara, kwani unakwenda sawa na kile ambacho Rais Samia anakitaka cha kuimarisha demokrasia nchini," anasema Ngawaiya.

> Kwa mtindo wa kupita bila kupingwa, maana yake ni kwamba baadhi ya wagombea wanakosa haki ya kuchaguliwa na pia wapigakura wanakosa haki ya kuchagua.

Anasema imedhihirisha jinsi inavyosimamia haki, kwa kuwa kulikuwa na njama za wazi zilizokuwa zikifanyika za kuzuia wagombea wengine wasichaguliwe an badala yake wale wasiotakiwa wanapata uongozi,

"Mfano, mgombea anachukua fomu lakini wakati wa kuirejesha anaambiwa msimamizi ameenda kujisaidia, anasubiri hadi usiku bila msimamizi kurudi au anaambiwa kuwa muda wa kupokea fomu umeisha, lengo likiwa ni kubeba baadhi ya wagombea," anasema.

Kada huo anasema ipo haja kwa mahakama kuendelea kuondoa sheria zote zilizokuwa kama kichaka cha kujificha wale wanaotafuta uongozi kwa ujanja ili kuimarisha utawala bora unaoutaka Rais Samia.

"Mimi ni kada wa CCM, lakini kwenye ukweli ni muhimu kuusema ili kusaidia wenzangu kuachana na mbinu ambazo wakati mwingine zinasababisha kupata viongozi ambao hawakubaliki," anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### WANAOSAKA HAKI

Dk. Anna Henga ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambaye anasema kwa uamuzi huo, sasa haki ya kuchagua na kuchaguliwa itapatikana.

Anasema mgombea kupita bila kupingwa ni sawa na kumnyima mpigakura haki yake ya kuchagua mtu anayemtaka amuongoze, na kwamba kila mtu ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

"Kwa mtindo wa kupita bila kupingwa, maana yake ni kwamba baadhi ya wagombea wanakosa haki ya kuchaguliwa na pia wapigakura wanakosa haki ya kuchagua," anasema Dk Anna.

Anasema yeye alikuwa miongoni mwa Watanzania walioumia katika uchaguzi wa serikali za Mitaa mwaka 2019 baada ya kwenda kupiga kura na kuambiwa kuwa mgombea amepita bila kupingwa.

Una uhakika gani kwamba huyo aliyepita bila kupingwa anapendwa? Tufike wakati sasa haki ya kuchagua au kuchaguliwa ichukue mkondo wake ili tupate viongozi tunaowataka," anasema.

### PENYE UTATA

Mwanasheria na pia Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema pamoja na uamuzi huo, lolote linaweza kutokea la kutokukubaliana na mahakama hiyo.

"Ilitakiwa iwe hivyo kwa mujibu wa sheria zetu, lakini kwa sababu ya kutokuwa na tume huru ndio maana kumekuwapo na viongozi wa aina hiyo kuanzia serikali za mitaa, madiwani na wabunge," anasema.

Anaongeza kuwa suala hilo pia bado lina utata, kwa madai kwamba inawezekana Mwanasheria Mkuu wa Serikali akakata rufaa kupinga uamuzi wa mahakama na hivyo akashinda.

Anafafanua kuwa uamuzi unaweza kukatiwa rufaa na mahakama ya juu nayo ikatengua, hivyo Watanzania wakajikuta wakiendelea kuwa ndani ya utaratibu wa baadhi ya wagombea kupita bila kupingwa.

"Binafsi ninapenda watu washindane siyo kubebwa, ili wananchi wapate viongozi wanaotaka, hivyo uamuzi huo ungeheshimiwa ingawa inawezekana ukakatiwa rufaa. Kwa mantiki hiyo siwezi kushangilia, kwa sababu lolote linaweza kutokea hasa kukatiwa rufaa," anasema.

### KESI ILIVYOKUWA

Mahakama ilifikia uamuzi huo katika hukumu yake ya kesi ya kikatiba, iliyofunguliwa na mwanasiasa, mwanachama wa chama cha ACT-Wazalendo, Joran Bashange, baada ya kukubaliana na hoja zake.

Bashange alifungua kesi hiyo Mahakama Kuu Masijala Kuu, Dar es Salaam, dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akipinga kuwepo kwa wabunge na madiwani wanaotangazwa kupita bila kupingwa.

Katika kesi hiyo ya kikatiba namba 19 ya mwaka 2021, Bashange alikuwa akihoji uhalali wa kikatiba wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Sura 343 kinachoruhusu kuwapo kwa wabunge wanaopita bila kupingwa.

Pia alikuwa akihoji uhalali wa kikatiba wa vifungu vya 45(5) na 13 (7) vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura 292 vinavyoruhusu kuwepo kwa madiwani wanaopita bila kupingwa.

Hukumu hiyo iliyotolewa na jopo la majaji watatu waliosikiliza kesi hiyo; John Mgetta (kiongozi wa jopo), Dk Benhajj Masoud na Edwin Kakolaki, mahakama hiyo inasema vifungu hivyo vinakinzana na Katiba.

Hivyo, inasema ni batili kwa kukiuka masharti ya Ibara ya 21(1) (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ambavyo imekuwa ikirekebishwa mara kwa mara.


# Miaka 39 bila ya Sokoine, ujasiri na uchapakazi wake ukibaki kuwa alama

Na James Kandoya

TANZANIA leo inatimiza miaka 39 tangu, kulipotokea kifo cha Waziri Mkuu wake, Edward Moringe Sokoine, aliyefariki kwa ajali ya gari eneo la Dakawa, mkoani Morogoro, akitoka kuhudhuria kikao cha Bunge mjini Dodomaa akielekea Dar es Salaam, katika eneo ambalo sasa ni wilayani Mvomero.

Ni kifo kilicholeta majonzi makubwa kwa Watanzania wa kawaida waliokuwa wanatarajia kuwatetea wanyonge na kuinua hali ya maisha ya wanyonge

Ni Waziri Mkuu wa Pili wa Jamhuri ya Muungano na wa tatu tukianzia na iliyokuwa Tanganyika, akirithi mikoba ya Rashidi Kawawa, aliyeshika madaraka hayo toka Februari 17 mwaka 1972 mpaka Februari 13 mwaka 1977.



Marehemu Edward Sokoine. Kushoto ni katika matukio tofauti, akiwa na Rais Julius Nyerere, picha nyingine katika tukio la kukagua gwaride. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



### UONGOZI WAKE

Uongozi wake ulionekana kuwa wa mfano kwa jinsi alivyokuwa na uadilifu, pia akiwa jasiri na kufuatilia utendaji kazi huku akikemea ulaji rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Haiba ya uongozi na msimamo wake ilitambulisha wazi kwa Watanzania ni kiongozi wa namna gani. Kwa ufupi, ni kiongozi ambaye hakupenda uzembe, uonevu, wizi na ubadhirifu wa mali za umma.

Mwaka mmoja kabla ya kifo chake, alitoa hotuba yake kufunga semina ya viongozi wa serikali na mashirika ya umma iliyopewa jina 'Uwajibikaji na Wajibu wa Viongozi' tarehe 26 Machi 1983, ambayo inashika rekodi ya namna yake jinsi ilivyobebna ujumbe mkubwa.

Hapo akataja baadhi ya mambo ya msingi kuzingatia. Hao akataja kasoro za kutofikia malengo au uzalishaji na utoaji huduma wa mashirika ya umma na kutaka kasoro ziangaliwe. Hapo akanena: "Tutafute kasoro zetu katika kila chombo tunachokiongoza, lazima tuanze sasa kupata ushindi na ufanisi katika sekta zote.Wananchi wamechoshwa kusikia hadithi za kushindwa kila siku."

Pia, anasema viongozi watakaoshindwa kuleta ufanisi katika maendeleo na usimamizi wao, iwapo hakuna sababu za kuridhisha kuwatetea wanapaswa ama kukaa kando au kurudishwa mstari wa nyuma, kwa kupunguziwa madaraka kama si kuondolewa, kwani umma unawategemea kushinda na si kushindwa.

Viongozi wa serikali na mashirika anawaambia lengo na shabaha za jamiii anakoelekea, ni kupata ushindi katika matatizo yao kwa kuzingatia uongozi na maelekezo ya chama na serikali kwa moyo na kauli moja ya kuishinda tutashinda.

Uhalisia huo, ndio sasa unarejesha kinachoripotiwa hata sasa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) na mashirika ya umma, imeonyesha mapungufu mbalimbali yamesababisha kutofikiwa malengo, kutokana na ubadhirifu wa wazi na uzembe.

> Tutafute kasoro zetu katika kila chombo tunachokiongoza, lazima tuanze sasa kupata ushindi na ufanisi katika sekta zote. Wananchi wamechoshwa kusikia hadithi za kushindwa kila siku.

Jambo lingine linalomrejesha katika fikra marehemu Sokoine, ni pale anaposisitiza ni kuhusu uongozi mbovu na uongozi duni au kuogopa kuamua kutekeleza mambo yaliyokubaliwa, akitumia hoja ingekuwa nafuu kufanya makosa katika kuamua, kuliko kufanya kosa la kutoamua.

"Chama na serikali kitakuwa tayari kuvumilia maamuzi yaliyofanywa na viongozi wa kazi, kwa nia njema lakini yana makosa, kuliko kukubali hatari ya kuwafanya watekelezaji katika wizara na mashirika ya umma, kuwa waoga kufanya maamuzi ama kuyatekeleza yale yaliyoamuliwa," anasema.

Anaongeza, viongozi wa mashirika ya umma wanapaswa kutambua kuwa chama na serikali vipo tayari kuelewa tofauti, kati ya maamuzi yanayofanywa kwa nia mbaya ya kulihujumu taifa na maamuzi ambayo yamefanywa kwa nia nzuri, ingawa yana makosa yasiyotazamiwa.

Ujumbe wa marehemu Waziri Mkuu Sokoine, unawakumbusha baaadhi ya viongozi wa chama na serikali wanaosahau kuwa hakuna hiari ya kuziheshimu sheria, wala hakuna mtu aliye juu ya sheria ni wajibu wa serikali kusimamia sheria.

### SAFARI YAKE

Marehemu Sokoine amehudumu kama Waziri Mkuu kwa vipindi viwili tofauti, kati ya Februari 13, 1977 mpaka Novemba 7, 1980 na madaraka kuchukuliwa na mrithi wake Cleopa Msuya, akitumikia nafasi hiyo hadi mwaka 1983.

Marehemu Sokoine, akarejea kwenye madaraka ya Waziri Mkuu mara ya pili, Februari 24 mwaka 1983 na mpaka April 12, 1984 alipofikwa na mauti. Ni baada ya hapo, utendaji mkuu wa serikali kwa nafasi hiyo ya Waziri Mkuu, ukachukuliwa na Salim Ahmed Salim, kuanzia Aprili 25, 1984 mpaka Novemba 5, 1985.

Wengine waliofuatia baadaye, ni Joseph Warioba, Novemba 5, 1985 mpaka Novemba 9, 1990, John Melecela, akachukua madaraka hayo akadumu nayo hadi Desemba 7, 1994 kwa mara ya pili, Cleopa Msuya akarejea nafasi hiyo, mpaka Novemba 24, 1995.

Wengine baada ya hapo ni Frederick Sumaye (Novemba 28, 1995 hadi Desemba 30, 2005), Edward Lowassa (Desemba 30, 2005 mpaka Februari 7, 2008); Mizengo Pinda (Februari 9, 2000 mpaka Novemba 30, 2008); kisha Kassim Majaliwa, tangu Novemba 20, 2015 hadi sasa.

### ANAVYOENDANA NA LEO

Katika miaka kadhaa iliyopo, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma, 2020/2021, kwamba ni uwazi kwa mashirika ya umma kwa 2020/2021 imeweka wazi upotevu mkubwa wa pesa za umma.

Ni ripoti inayotoa mapendekezo na hatua za kuchukuliwa, ili kudhibiti vyanzo vya upotevu huo ikiwamo uzembe, ubadhirifu na kutoa mapendekezo kwa serikali, namna bora ya kudhibiti, ikiwamo kuchukua hatua kwa viongozi wazembe.

Ikiangaliwa misingi ya hoja yake, ikiwamo ya mwaka mmoja kabla ya kifo chake, haja uwajibikaji na uamuzi wa kiongozi. Sasa ni kitaalamu, inatajwa kuwa wakati mwafaka hilo kufanyika, kwa serikali kuchukua hatua za makusudi dhidi ya watendaji wabovu na wazembe kwa kuwaengua wasiofaa baada ya kujiridhisha.

Serikali iwape nafasi na kuwatia shime viongozi waondokane na uoga wa kufanya maamuzi kwenye taasisi zao au utekelezaji wa maelekezo kutoka mamlaka za juu.

Ni ujumbe unaoenda mbali, kutaka kuchukuliwa hatua dhidi ya viongozi wabadhirifu na wazembe. Kwa mashirika ya umma na kiserikali kutokuwa na woga kufanya maamuzi stahiki.

### HISTORIA BINAFSI

Marehemu Sokoine alizaliwa mwaka 1938 wilayani Monduli, mkoa wa Arusha na akaendelea na sekondari ya Umbwe mkoani Kilimanjaro, alikohitimu mwaka 1958. Baadaye mwaka 1961, ndipo alipojiunga rasmi na chama cha TANU, na baada ya hapo akapata mafunzo ya utawala nchini Ujerumani, kati ya mwaka 1962 na 1963.

Baada ya kurejea nchini, akateuliwa kikazi kuwa Katibu Mtendaji wa Wizara ya Mawasiliano, Usafiri na Kazi. Baada ya miaka mitatu. 1970 alipandishwa kuwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mwaka 1972.


Ilipofika mwaka 1977,wakati huo CCM ndio imezaliwa,akateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, huku akiteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

JUKWAA LA VIONGOZI

MJUE OSCAR KAMBONA

# Mchangia uhuru aliyekimbia nchini miaka michache baada kuwa waziri

• Miaka 5 baada ya kurejea siasa za nyumbani, akafariki



Oscar Kambona, akiwa na Rais Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KIMSINGI inapotajwa historia ya nchi na hasa kisiasa, kuna majina ambayo ni magumu kutotajwa kwa namna moja au nyingine. Hapo kuna Oscar Kambona.

Huyo safari yake kimaisha ina namna inavyoshabihiana na nyendo za marehemu, Rais Julius Nyerere. Kimsingi, nyayo zake zinaenda mbali ikianzia na simulizi yake binfasi, alivyoweza kumshawishi askofu amlipie ada.

Baada ya kumaliza masomo ya sekondari aliendа katika shule kama mwalimu na baadae alichaguliwa kuwa mkuu wa shule. Hapo ndipo, wakiwa katika mkutano wa kitaifa wa walimu, mwaka 1954, Kambona na Nyerere walikutana.

Kambona alikuwa tayari anakitumikia chama cha TANU, ambacho kilikuwa kimeanzishwa muda si mrefu, lakini Nyerere akasema wasingeweza kumwajiri kwa vile chama kilikuwa hakina fedha.

Inaelezwa wakakubaliana naye akisema ni kweli, chama chao hakikuwa na fedha kwa vile hakikuwa na katibu mtendaji wake na ndipo alipoamua kufanya kazi hiyo ili kujenga chama, bila ya malipo. Hapo akaishi kwa kutegemea akiba aliyojitunzia kwa kufanya kazi miezi sita.

Ni katika kipindi hicho, Kambona akasafiri sehemu mbalimbali za nchi kuanza kampeni, akionana na machifu na wazee wa vijiji, waanze kusajili wanachama. Ni kweli katika miezi sita, akafanikiwa kusajili wanachama 10,000 na hadi kufikia mwaka mmoja alikuwa amepata wanachama hai 100,000.

Kambona ametumia michango

> Hatimaye maasi hayo yalidhibitiwa kabisa na majeshi ya Uingereza na Nyerere alimsifu Kambona busara na uaminifu wake. Tofauti kati ya Nyerere na Kambona zilianza kujitokeza baada ya maasi ya wanajeshi.



aliyopata kufungua akaunti ya kwanza ya chama TANU na kisha akaenda Butiama kujadiliana na Rais Nyerere achukue uongozi wa kudumu wa chama. Baada ya miaka mitatu akaamua kwenda kusomea sheria nchini Uingereza mwaka 1957, kwa ufadhili wa Gavana Edward Twining wa wakati huo,

Vilevile ni kipindi ambacho nyendo za TANU zimeshika kasi, Rashid Kawawa aliyeanzia kwenye chama cha wafanyakazi, Tanganyika Federation of Labour (TFL), akiwa katika safu ya juu ya mapambano kusaka maslahi ya uhuru wa Tangayika, baada ya kushawishiwa na Mwalimu Nyerere.

Akiwa masomoni jijini London, Kambona hakubweteka, akaendeleza siasa zake za nyumbani Tanganyika, akiwa kiongozi wa Chama cha Wanafunzi wa Tanganyika, vilevile Mwenyekiti wa tawi la TANU, jijini London.

Ni wakati huo ambao Kambona akapata fursa ya kukutana kwa mara ya kwanza na watu mashuhuri wa huko, akiwamo George Padmore, mwanaharakati wa Umoja wa Afrika, hata akamshawishi ahudhurie mkutano wa mwaka 1958 wa Waafrika Wote, uliofanyika nchini Ghana muda mfupi baada ya kupata Uhuru.

Akiwa nchini Ghana, Kambona akapata nafasi ya kukutana na mwanaharakati mwingine maarufu wa siasa za Afrika, Dk. Kwame Nkurumah na akiwa nchini Uingereza Kambona, akaweka historia kuwa Mwafrika wa kwanza kutangaza taarifa ya habari kwa lugha Kiswahili, katika Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC).

Baada ya kurudi nchini mwaka 1959, TANU ilikuwa imeshakuwa imeweka bayana madai yake ya kupewa serikali ya madaraka, vinginevyo ilikuwa tayari kuanzisha mapambano kama ilivyokuwa kwa majirani kama chama cha Mau Mau ya Kenya.

Wakiwa jijini London wakisubiri kupewa Madaraka ya Ndani, Mwenyekiti wa TANU, Nyerere akiwa na Kambona, walijadili hatua mbalimbali ambazo zingechukuliwa kuepuka kutoweka amani nchini Tanganyika, hata anakumbukwa na waandishi wa habari mjini Londoni 1991, akirejea matukio kwa kunena 'Bwana Nyerere alikuwa akiishi nami katika chumba kidogo nilichopewa chuoni."

Katika harakati hizo za matayarisho ya serikali ya ndani, Kambona alifunga ndoa ma mke, Flora Moriyo, huku akiendelea na harakati za kupata Uhuru, jijini London, katika tukio ambalo Mwalimu Nyerere, ndiye alikuwa msimamizi wa Kambona.

Baada ya uhuru, Kambona akateuliwa kuwa waziri mwandamizi akiongoza Wizara ya Elimu, pia baadaye Mambo ya Ndani, Mambo ya Nchi, Mambo ya Nje, Ulinzi, pia Tawala za Mikoa.

Pia, Kambona alishakuwa Mwenyekiti wa Kwanza wa Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika, akaongoza uandaaji mwongozo wake, huku mwaka 1964, anatajwa kuwa na mchango mkubwa katika jukumu la kuandaa muunganiko kati ya Zanzibar na Tanganyika, kuunda Tanzania, chini ya Rais Nyerere na Makamu, Sheikh Abeid Amen Karume.

Hatimaye maasi hayo yalidhibitiwa kabisa na majeshi ya Uingereza na Nyerere alimsifu Kambona busara na uaminifu wake. Tofauti kati ya Nyerere na Kambona zilianza kujitokeza baada ya maasi ya wanajeshi.

Kimsingi, hoja ya kuanzishwa chama kimoja iliyosistizwa na Mwalimu Nyerere, Kambona hakukubaliana nayo sana, hata wakaingia kwenye tofauti iliyofika sura pana ya msuguano kiserikali, hata baadae akakimbia nchini akielekea Uingereza, kupitia nchi jirani ya Kenya.

Wakati wa mageuzi ya kisiasa nchini, mfumo wa vyama vingi ukiwa umerejea, mwanzoni mwa miaka ya 1990, Kambona akitumaini kuwapo makubwa ya mabadiliko ya kisiasa, akaunda chama kiitwacho Tanzania Democratic Alliance. Ni wakati huo akatua nchini akitumia pasi ya Uingereza , miezi miwili huku kukiwa kumeanzishwa rasmi mfumo wa vyama vingi Tanzania, mnamo Julai1992.

Hakuchukuliwa hatua, akipewa miezi mitatu awe amekamilisha kilichotajwa 'utata wa uraia wake.'Hata hivyo Kambona hakuweza kujihusisha kwa kiasi kikubwa na siasa kutokana na hali duni ya afya yake kwenye shinikizo la damu na akafariki dunia, akiwa katika matibabu jijini London, Juni 1997.

***• Kwa mujibu wa taarifa zake mbalimbali za kihistoria.***



## Simbachawene azindua mpango mkakati WFP

**Na Renatha Msungu,**DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amezindua Mpango Mkakati wa mwaka 2022-2027 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) unaotarajia kutumia Dola za Marekani milioni 363.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Jenista Mhagama, Simbachawene alisema mpango mkakati huo unalenga kuboresha masuala mbalimbali yakiwemo kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na maafa kabla hayajatokea.

Waziri Simbachawene alisema Mpango huo utawezesha utekelezaji wa Mpango wa Lishe kwa jamii na mpango wa chakula shuleni ikiwemo kukuza jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na urejeshaji hali ya mazingira.

"Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu ni wazi utasaidia kuwainua wakulima wadogo ili kuongeza tija katika uzalishaji na kuwawezesha kupata masoko ya mazao.

Katika eneo hili WFP itawasaidia wakulima kuwa na utaratibu bora wa kutunza mazao kabla kuyafikisha sokoni (Post Harvest strategies) na kutoa elimu kwa wakulima ," alisema Simbachawene.

Waziri pia alizitaka wizara, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zitakazonufaika na utekelezaji wa mkakati huo kushirikiana na WFP ili kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa na kuchangia katika kuboresha hali za maisha ya watu.

Hata hivyo alisema uzinduzi huo unafuatia kukamilika kwa Mpango Mkakati wa WFP uliotekelezwa kwa kushirikiana na serikali tangu mwaka 2017-2021 huku akisisitiza serikali inatambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na wadau katika kuchangia maendeleo ya nchi.

Katika hatua nyingine, Simbachawene ameeleza kwamba mkakati huo utawezesha nchi kufikia malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 ambayo yamejikita katika kupunguza umasikini na kuleta ustawi wa maisha ya watu.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson, aliishukuru serikali ya Tanzania kwa usaidizi, uaminifu na ushirikiano wake huku akiahidi kuwa WFP itahakikisha Tanzania inakuwa nchi endelevu na yenye uwezo wa kustahimili maisha bora kwa Watanzania wote.

Alisema ushirikiano huo utaendelea ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea katika kupunguza umaskini.

# Manyoni yaanza kampeni kuondoa baa la njaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WILAYA ya Manyoni mkoani Singida imeandaa mpango wa kutokomeza baa la njaa katika wilaya hiyo kwa kuanzisha kampeni maarufu kama Ondoa Njaa Manyoni (ONJAMA).

Kampeni hiyo itakuwa na jukumu la kuhamasisha wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame kulingana na jiografia ya eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemilembe Lwota, alitangaza kuanzishwa kwa kampeni hiyo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Itigi.

Alisema serikali imekuwa ikifanya kazi nzuri ya kuwapatia wananchi chakula cha bei nafuu katika maeneo yenye njaa ikiwamo wilaya ya Manyoni lakini akasisitiza kuwa utaratibu huo wa kutegemea serikali kuwapatia chakula hauna budi ufike kikomo.

Lwota alisema pamoja na jografia ya wilaya hiyo kuwa na mvua zisizotabirika bado wananchi wanaweza kulima mazao ya chakula kama mihogo, mtama, uwele na mazao mengine ambayo yanaweza kuhimili mvua chache.

Aliongeza kuwa madiwani wana nafasi nzuri ya kwenda kuhamasisha wananchi katika maeneo yao kulima mazao yanayohimili mvua chache ili kuepuka baa la njaa kujirudia katika wilaya hiyo.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwataka madiwani, divisheni ya elimu na viongozi wa ngazi ya kata kuhakikisha wanafunzi wote wanaotakiwa kuwa shuleni katika hatua ya elimu ya msingi na sekondari kuripoti shuleni mara tu shule zitakapofunguliwa.

Alisisitiza kuwa serikali imefanaya kazi kubwa ya kujenga miundombinu bora ya elimu ikiwemo vyumba bora na vya kutosha vya madarasa lakini changamoto imebaki katika zoezi la uandikishaji wa wanafunzi na kusema kuwa jambo hilo halikubaliki.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba, akifungua kikao hicho, alisema halmashauri kwa kiwango kikubwa inategemea makusanyo yanayotokana na mazao ya kilimo na hadi kufikia sasa makusanyo ni takribani Sh. milioni 894 sawa na asilimia 47.

Simba alibainisha mikakati ya kuongeza vyanzo vingine vya mapato vikiwamo kujenga maegesho ya maroli na stendi ya magari katika mji wa Itigi na stendi ya magari katika kata ya Rungwa ambayo ujenzi wake unaendelea na mpaka sasa umegharimu Sh. milioni 30.



Mbunge wa jimbo la Mvumi, Livingstone Lusinde akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wataka waliobainika kuhusika na ufisadi ripoti ya CAG wawajibike

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UMOJA wa Madhehebu ya Kikristo mkoani Dodoma umetoa tamko la kumshauri Rais Samia Suluhu Hassan kuwachukulia hatua kali na kuwafuta kazi wateule wake ambao watabainika kujihusisha na ufisadi wa mali za serikali kama ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilivyobainisha.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Umoja wa huo. Askofu Anthony Mlyashimba wa Kanisa la Baptisti kwenye ibada ya Jumatatu ya Pasaka iliyofanyika Kanisa Kuu la Anglikana, Dodoma.

Mwenyekiti huyo alisema ni aibu kwa serikali kuona watumishi wake ambao wanatakiwa kulinda mali walioaminiwa na Rais wanakuwa vinara wa kufanya ufisadi wa kutisha na kueleza kuwa hii ni aibu kwa taifa.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema kuwa umoja huo unalaani ukiukwaji huo wa maadili kwa baadhi ya watumishi wa umma wanaofanya ufisadi kwenye sekta zao wanazofanyia kazi.

"Sisi Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma tunamuunga mkono Rais Samia kwa kukemea hadharani uozo huo kwa wale wote watakaobainika kufanya ufisadi.

"Tunaomba Rais kuchukua hatua kali na stahiki kwa watumishi wote waliosababisha ubadhilifu huo. Kama wameshindwa wao wenyewe kuwajibika basi Rais mwenyewe awawajibishe," alisema.

Askofu Mlyashimba alisema akilini watu wamesababisha matatizo makubwa kwa nchi na bado wako maofisini tu wanaendelea kufanya kazi, hii ni dharau kwa ofisi ya Rais na kwa Watanzania wote.

"Hivi kwa mfano madudu yaliyofanyika Bohari Kuu ya Dawa (MSD), dawa zenye thamani ya Sh. milioni 235.84 zimeharibika huku hospitali, vituo vya afya na zahanati zetu wagongwa wanaambiwa hakuna dawa na wakanunue kwenye maduka ya dawa. watumishi waliosababisha hayo yote kweli wanastahili wakae ofisini? Alihoji.

Pia alitaja Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) ambalo linadai Sh. bilioni 21 na hawajui wanamdai nani haikubaliki, hivyo wanamwomba Rais alisaidie taifa kwa kuwaondoa wahalifu hao kazini ili fedha zinazopotea zisaidie Watanzania wote.

Askofu wa Kanisa la Africa Inland Tanzania, Dayosisi ya Kanda ya Kati, Amos Katoto, alisema serikali inatakiwa kuangalia mifumo inayoingizwa kutoka kwa baadhi ya wageni kutoka nchi za Ulaya mingine inakuja kwa malengo vitendo visivyofaa kama vile vya ushoga, ulawiti usagaji na ndoa za jinsia moja.

Alisema mifumo hiyo imekuwa machukizo mbele za Mungu na kutaka kanisa lisimame imara kukemea vitendo hivyo na asiwapo mtu yoyote wa kuviunga mkono.

Askofu huyo pia aliutaka umoja huo wa makanisa ya madhehebu ya Kikristo kufanya kazi kwa uaminifu, kuhubiri neno la kweli ambalo halina upotoshaji ndani yake na kushirikiana serikali kwenye mambo ya maendeleo.





# Kiongozi Wasafwa acharuka ushoga

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KIONGOZI wa kabila la Wasafwa mkoani Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, amewataka viongozi wenzake kushirikiana na Serikali kuwabaini watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja, ulawiti na ubakaji wa watoto kisha kuwachukulia hatua.

Chifu Mwashinga amesema matendo hayo yanakwenda kinyume cha mila na desturi za Kitanzania, hivyo yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo, apewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano uliowahusisha machifu kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya ikiwa ni maandalizi ya uzinduzi wa tamasha la kabila hilo litakalofanyika Oktoba, mwaka huu.

"Ni aibu katika sisi wazazi tuliozaa kuona matendo kama haya. Ningekuwa kiongozi serikalini ningewapiga wote risasi wapotee. Mila na desturi zimedharaulika siku hizi kwa sababu ya kuiga mtindo wa maisha ya nchi za wenzetu," alisema.

Kiongozi huyo aliiomba jamii kushirikiana na viongozi wa maeneo mbalimbali kuanzia serikali za mitaa, vijiji na kata kutoa taarifa wanapobaini au kuwaona watu wa namna hiyo, sambamba na kuisihi serikali kuwashughulikia kwa mujibu na sheria za nchi.

Baadhi ya wazazi wamekiri kuwa sehemu ya kuchangia mmonyoko wa maadili kwa kusahau au kupuuza kutimiza wajibu wao katika malezi ya watoto na kujikita kwenye shughuli za uzalishaji mali.

Boniface Mwalwego alisema hali hiyo imechangia kushamiri kwa vitendo hivyo ambavyo vinadhalilisha utu wa mwanadamu na kusahau kuwafundisha watoto umuhimu wa kulinda na kuenzi mila na desturi za asili katika makabila yao.

Mwalwego alisema mabadiliko ya sayansi na teknolojia yamechangia kwa kiasi kikubwa mmomonyoko wa maadili huku wazazi wakiwaruhusu watoto wakiwa na umri mdogo kumiliki na kutumia simu, kuangalia tathmilia au nyimbo ambazo hazina maadili.

"Baadhi ya wazazi wanajifanya wanaishi kisasa. Wanawalea watoto wao pasipo kufuata misingi na taratibu za nchi badala yake wanajifunza mambo yasiyofaa na kusababisha kuzalisha kizazi kilichokengeuka. Hatujachelewa, tujisahihishe tuendelee kulea watoto katika maadili yanayofaa pamoja na kuwaadhibu ili kurudi kwenye mstari," alisema Mwalwego.

Cosmas Julius kwa upande wake alisema wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto namna ya kuwatambua marafiki wabaya na kuwaepuka ili kutojiingiza kwenye tabia zisizofaa.

Mtaalam wa Saikolojia, Joshua Lawrence, alisisitiza mtoto kujengewa misingi mizuri katika umri wa miaka kuanzia 0-12 ili kusaidia mwelekeo wake wa baadaye na kwamba mzazi akifeli eneo hilo atavuna matokeo mabaya kwa mtoto wake.

Aliwasisitiza wazazi pamoja na walezi kuzingatia malezi na makuzi kwa watoto wao ili kuwaepusha na tabia hatarishi hapo baadaye ambazo zinaweza kuharibu ndoto za maisha yao.



Kiongozi wa Kabila la Wasafwa mkoani Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, akizungumza katika mkutano wa kujadili mambo mbalimbali yanayohusu kabila hilo ikiwemo tamko la kukemea vitendo vya mapenzi ya jinsia moja, ulawiti na ushoga, katika viwanja vya Ruanda Nzovwe juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanafunzi hatarini magonjwa ya mlipuko

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANAFUNZI wa kike katika Shule ya Sekondari Kalobe jijini Mbeya, wako hatarini kupata magonjwa ya mlipuko baada ya vyoo walivyokuwa wakitumia kubomoka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Mbeya.

Kwa sasa wanafunzi hao 453 wanalazimika kujisaidia kwenye nyumba za majirani wanaozunguka shule hiyo huku wakisubiri ujenzi wa vyoo vipya ukamilike.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kalobe, Songa Halson, alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo, alitoa taarifa kwa bodi ya shule na kukubaliana kukatisha masomo kwa muda ili kulinda afya za wanafunzi hao.

Alisema kikao kiliazimia shule isifungwe badala yake wanafunzi wa kike waendelee kutumia vyoo vya walimu wa kike ambavyo ni matundu mawili kwa muda na kwamba tayari uchimbaji wa shimo kwa ajili ya vyoo vipya ulianza na ujenzi unaendelea.

"Baada ya tathmini kufanyika tulikubaliana kujenga vyoo vipya zaidi ya matundu 320 ambavyo gharama yake itakuwa Sh milioni 69 mpaka kukamilika kwake na kwamba wataalam wametuahidi kuzingatia ubora ili tatizo hili lisijirudie tena," alisema.

Baada ya kupata taarifa ya vyoo vya shule kubomoka, Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye pia ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alitoa mifuko 100 ya saruji.

Aliongeza kuwa msaada huo ni sehemu ya kutoa pole na kusaidia ujenzi wa vyoo vingine ili kunusuru afya za wanafunzi hao.

Irene Mtambo, mwanafunzi wa kidato cha tatu, alisema mvua kubwa iliyoambatana na radi ilibomoa vyoo hivyo na kusababisha usumbufu kwa wanafunzi hao kutafuta maeneo mengine ya kujisaidia.

Alisema tatizo hilo walilibaini walipokuwa wakifanya usafi kwenye mazingira ya shule na baadae wakapata taarifa kutoka kwa mkuu wa shule.

Betilda Mwasobye alisema baada ya kupewa taarifa na mkuu wa shule wakalazimika kurudi nyumbani kwenda kuwajulisha wazazi wao na kuhitajika kwa ajili ya kujadili namna ya kufanya ili kujenga vyoo vipya.

Alisema mzazi wake alimuambia wamekubaliana kujenga vyoo vipya kwa dharura ili kusaidia watoto adha ya kukosa vyoo isiwe kwa kipindi kirefu.

## RC Homera ageukia utunzaji vyanzo maji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameitaka sekta ya maji kutoa elimu kwa wananchi umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi endelevu ya maji.

Pia amesisitiza umuhimu wa wadau kutoa elimu ya sera ya maji kwa kuwa ndio mwongozo wa kutekeleza majukumu yao ya kumtua mama ndoo kichwani, suala ambalo ni ajenda ya serikali kwa sasa.

Homera alisema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wadau wa sekta ya maji baada ya kutembelea mabwawa ya majitaka katika kata ya Kalobe jijini Mbeya.

Alisema sekta ya maji ina wadau wengi, hivyo ni vyema wakashirikiana kuhakikisha wanatoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa kuwa dunia kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa mkoa alisisitiza kuwa kwa sasa serikali imedhamiria kumtua mama ndoo kichwani, hivyo ni jukumu la wadau wa sekta ya maji kuwaeleza mipango hiyo ili kusaidia rasilimali hiyo kutunzwa.

"Nawaagiza UWSA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya), RUWASA (Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini) na watu wa wa Bonde la Ziwa Rukwa nendeni kwa wananachi muwaeleze sera ya maji inasema nini. Lakini mtoe elimu ya uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji ili wananchi watambue kuwa ni sehemu ya utunzaji wa mazingira hususani kwenye kipindi hiki tunachabiliana na suala la mabadiliko ya tabia nchi" alisema Homera.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya UWSA, Simon Bukuku, alisema katika kuhifadhi na kutunza mazingira wamepanga kupanda miti 3,000 ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Alifafanunua kuwa eneo la Kalobe walipanda miti 150 na kwamba wataendelea kupanda maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji ili kuendelea kutunza ikolojia na uoto wa asili kuzunguka maeneo hayo.

Mkazi wa Kalobe, Fadhil Matiko, alisema wataendelea kushirikiana na mamlaka za maji kutunza vyanzo ambavyo vinasaidia upatikanaji wa maji maeneo wanayoishi.





## Hemed asisitiza shule za ghorofa

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar , Hemed Suleiman Abdulla amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kujenga shule za ghorofa kwa lengo la kuwawekea wanafunzi mazingira mazuri ya kusomea ili kukuza ufaulu nchini.

Hemed aliyasema hayo juzi wakati akikagua ujenzi wa jengo la shule lenye ghorofa tatu linalojengwa na kampuni ya Mwinyi Building lililopo Kiwani mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema serikali inaendelea kujenga shule za ghorofa za kisasa zinazoendana na wakati hali ambayo itasababisha upatikanaji wa elimu bora kwa ngazi zote nchini.

Hemed alimtaka mkandarasi huyo kuendelea kutunza imani aliyopewa na Ssrikali na kwa kusimamia ujenzi huo kwa ufanisi ili kukamilisha mradi huo kwa kiwango na kwa wakati uliopangwa.

Alisema serikali imeamua kujenga shule 21 za ghorofa kwa mwaka huu na Kiwani ni miongoni mwa shule hizo majengo ambayo yatatatua uhaba wa madarasa na kufikia lengo la wanafunzi kuingia mkondo mmoja kwa Unguja na Pemba, hivyo kufanya vizuri katika masomo yao.

Hemed aliwataka wananchi wa maeneo hayo kutoa ushirikiano kwa mkandarasi huyo ili kumwezesha kukamilisha kazi kwa wakati.

Mshauri Mwelekezi wa ujenzi huo, mhandisi Farhat Masoud Ali, alisema mradi huo ulianza Aprili 5, mwaka huu, na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu na kwamba utajumuisha madarasa 42, vyoo 29, maabara tatu, ofisi za walimu, chumba cha kompyuta na kumbi za mikutano.

# Wizara yasisitiza ahadi za Rais ujenzi barabara zinatekelezwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, inaendelea na usimamizi kuhakikisha ahadi zilizotolewa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, za ujenzi wa miundombinu ya barabara zinatekelezwa.

Katika kusimamia utekelezaji huo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, akiwa na viongozi wingine wa wizara wamefanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ambazo zinaendelea kujengwa.

Waziri katika ziara hiyo, amekagua maendeleo ya ujenzi kwa barabara ya Jozani-Charawe-Ukongoroni yenye urefu wa kilomita 23.

Pia Waziri amekagua barabara ya Mchangamle kuelekea hoteli ya Residence, ambayo itasaidia kuinua uchumi kupitia utalii, sambamba na maendeleo ya barabara Dunga- Mgeni Haji pamoja na barabara za Mwakaje, Mwachealale na Bumbwisudi ambazo zitasaidia kuinua kipato cha wananchi kupitia sekta ya kilimo.

Akiwa katika ziara hiyo, waziri alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi kwa barabara ya Jozani – Charawe- Ukongoroni inayojengwa na kampuni ya URKUM kutoka Uturuki.

Akizungumza na makandarasi wa barabara zinazojengwa na kampuni ya IRIS ASER, Waziri Dk. Khalid aliwataka kukamilisha kilomita 170 walizokubaliana na uongozi wa wizara hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu.

Pia Waziri Khalid aliitaka kampuni ya IRIS ASER kuhakikisha inaanza ujenzi wa barabara kwa upande wa Pemba.

Msaidizi msimamizi wa mradi kutoka kampuni ya IRIS ASER, Malik, alimhakikishia waziri kilomita hizo zitakamilika na kumweleza kuwa tayari kampuni imeshapeleka watendaji wake Pemba kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara za Kisiwa cha Pemba.

Wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo mradi wa barabara hizo umepita wamemshukuru Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa kuhakikisha ahadi alizozitoa zinakamilika na kuanza kwa harakati hizo za ujenzi maisha ya wananchi yameanza kufunguka kutokana na baadhi ya watu wameanza kuwekeza katika maeneo mbalimbali.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (kulia), akikabidhi mabati 80 kwa Makame Simai, kwa ajili ya ujenzi wa Msikiti ulioathirika na upepo mkali, Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabadiliko sheria kudhibiti uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu imesema marekebisho ya Sheria ya Uvuvi namba 10 ya mwaka 2010 lengo lake kubwa ni kuweka mkazo katika kulinda mazingira ya baharini na rasilimali zake pamoja na kupambana na uvuvi haramu ambao ni tishio kwa viumbe vya baharini.

Katibu Mkuu wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema hayo jana alipozungumza na wavuvi na viongozi wa kamati za uvuvi za hifadhi ya ghuba ofisini kwake mjini Zanzibar.

Alisema sera ya uchumi wa buluu dhana yake kubwa imejikita katika kulinda mazingira ya baharini na rasilimali zake ikiwamo kupambana na uvuvi haramu.

Jumbe alisema uvuvi haramu haukubaliki katika uchumi wa bluu na katika sheria mpya ya uvuvi imebainisha aina ya uvuvi ambao unakubalika.

Alisema hadi sasa bado wako wavuvi ambao wanaendeleza uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi, hivyo kutishia maisha ya baadhi ya samaki ambao wako katika tishio la kutoweka.

"Katika sheria mpya za uvuvi tumebainisha aina ya uvuvi unaokubalika na ule ambao tumepiga marufuku kutokana na kuwapo kwa tishio la athari ya mazingira ikiwamo uharibifu wa matumbawe," alisema.

Dk. Jumbe alitaja baadhi ya njia za uvuvi ambazo zimepigwa marufuku ni wa kutumia nyavu zenye macho madogo za kukokota ambazo ni tishio kwa mazingira ya bahari ambazo zimekuwa zikivua samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Alisema serikali ya Zanzibar inatarajiwa kutekeleza mradi wa heshimu bahari unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia Shirika la Misaada la Kimataifa (USAID) ambao umejikita moja kwa moja katika kulinda mazingira ya bahari katika maeneo ya hifadhi za bahari na kuona uvuvi unakuwa endelevu.

Baadhi ya wavuvi na viongozi wa kamati za uvuvi za hifadhi walisema sheria mpya ya uvuvi inahitajika ambayo itaweka mikakati ya kupambana na uvuvi haramu ikiwemo katika maeneo ya hifadhi ambayo yanalindwa kwa mujibu wa sheria za hifadhi.

Aidha Haji Ame Pakacha, kiongozi wa hifadhi ya uvuvi ya Minca, alisema baadhi ya samaki adimu wameanza kutoweka wakiwemo ngisi, pweza na kamba kutokana na kasi ya uvuvi ambao unachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazingira hususani matumbawe.

Zaidi ya wavuvi 34,000 wamejiajiri katika sekta ya uvuvi ana jumla ya tani 24,000 za samaki huvuliwa kila mwaka na kuingiza wastani wa Sh. bilioni 36.

## HABARI KIMATAIFA

MAANDAMANO KENYA;

# Chama tawala kujadili hoja za upinzani

**Nairobi,** KENYA

WABUNGE wa muungano unaotawala nchini Kenya wamekutana leo na kuchagua timu ya kujadiliana na upinzani, kuhusu gharama ya maisha na masuala mengine yaliyosababisha maandamano ya wiki kadhaa mwishoni mwa mwezi Machi.

**Upinzani ulikuwa umesitisha maandamano ya Aprili 2...**

Muungano huo wa Kenya Kwanza, umechagua ujumbe wake wa watu saba kwenye mazungumzo ya wabunge wa pande mbili na upinzani.


Wakati wa mkutano na wanahabari katika Ikulu, Jumanne, Kiongozi wa Wengi katika Bunge la Kitaifa, Kimani Ichung'wa alisema wabunge hao walichaguliwa baada ya majadiliano wakati wa mkutano wa awali wa Kikundi cha Wabunge wa Kenya Kwanza.

Kiongozi wa upinzani Raila Odinga, Aprili 4, mwaka huu, alitishia kuitisha maandamano mapya iwapo serikali itashindwa kuyachukulia kwa uzito mazungumzo hayo.

Upinzani ulikuwa umesitisha maandamano ya Aprili 2, mwaka huu, baada ya Rais William Ruto kuitisha mazungumzo.

Muungano wa Azimio la Umoja wa Odinga, One Kenya na umetaja timu ya watu saba kwa ajili ya majadiliano hayo.

Umoja huo, unaitaka serikali kuchukua hatua za kupunguza gharama ya maisha, kufanya mageuzi ya uchaguzi, kufungua seva za tume ya uchaguzi na kuacha kuajiri maofisa wa wakala wa kura. **BBC**



Rais William Ruto (kulia) na mpinzani wake Raila Odinga. **PICHA:MTANDAO**

## Mwanamume aua watu watano kwa risasi benki

**Louisville,** MAREKANI

WATU watano wamefariki dunia wakati mfanyakazi mmoja wa benki mjini Louisville, Kentucky alipowashambulia kwa risasi polisi imesema.

Waathiriwa walikuwa na umri kati ya miaka 40 na 64. Miongoni mwa watu tisa waliojeruhiwa, alikuwamo ofisa wa polisi ambaye alikuwa amemaliza mafunzo wiki mbili zilizopita. Ofisa huyo alipigwa risasi kichwani, anmefanyiwa upasuaji wa ubongo.

Polisi walifika katika eneo la tukio katika muda wa dakika tatu na kumpiga risasi mshambuliaji ambaye alifariki katika makabiliano ya risasi. Shambulio hilo lilifanyika katika benki ya zamani katikati mwa jiji.

Caleb Goodlet, aliviambia vyombo vya habari kwamba mke wake, ambaye ni mfanyakazi wa benki, alijifungia ndani ya jengo wakati shambulio lilipoanza.

Watu wengine walioshuhudia walielezea ufyatulianaji risasi kati ya maofisa wa polisi na mshambuliaji. **BBC**

## Russia,Ukraine waachiana wafungwa

**Moscow,** RUSSIA

RUSSIA na Ukraine zimebadilishana zaidi ya wanajeshi 200 katika mabadilishano ya hivi karibuni ya wafungwa, maofisa wamesema.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, imesema wanajeshi wake 196 waliachiliwa huru kutoka gereza la Ukraine.

Andriy Yermak, mkuu wa utawala kwenye ofisi ya Rais Volodymyr Zelenskiy, alisema Russia iliwaachilia huru wafungwa 100 wa Ukraine.

Hakuna tangazo lililofichua maelezo ya jinsi ubadilishanaji wa wafungwa ulivyotekelezwa.

Yermak alisema kwenye mtandao wa Telegram kwamba, baadhi ya wanajeshi wa Ukraine wana majeraha mabaya na magonjwa.

Alisema ubadilishanaji wa wafungwa wa hivi karibuni katika vita vya miezi 14, haukuwa rahisi ingawa hakutoa ufafanuzi.

Ubadilishanaji wa wafungwa, ni mojawapo ya mambo machache ambayo Ukraine na Russia zinashirikiana na kukubaliana. **VOA**

## Ufilipino, Marekani zafanya luteka kubwa

**Manila,** UFILIPINO

UFILIPINO na Marekani, zimeanza mazoezi makubwa ya kijeshi ya pamoja, ambayo hayajawahi kufanyika katika eneo la nchi hiyo ya Kusini Mashariki mwa Asia.

Wachambuzi wa masuala ya kimataifa wanatafsiri luteka hiyo ya washirika hao wa muda mrefu kwamba, ni kujaribu kukabiliana na ushawishi unaoongezeka wa China katika eneo hilo.

Wanajeshi 18,000 wa Marekani na Ufilipino watashiriki katika mazoezi hayo, yatakayochukua muda wa wiki mbili. Mazoezi hayo yatajumuisha kwa mara ya kwanza zoezi la urushaji risasi za moto katika Bahari ya Kusini mwa China, ambayo Beijing inadai kuwa ni milki yake.

Mojawapo ya mazoezi hayo, yatashirikisha kutua kwa helikopta za kijeshi kwenye kisiwa cha Ufilipino kwenye pwani ya kaskazini mwa kisiwa kikuu cha Luzon, karibu kilomita 300 kutoka Taiwan.

Uzinduzi wa mazoezi haya ya kila mwaka ya Balikatan, neno linalomaanisha bega kwa bega, kwa Kifilipino, unakuja baada ya operesheni ya kijeshi ya siku tatu iliyohitimishwa Jumatatu Aprili 10, mwaka huu na Beijing.

Mashambulizi yalijumuisha kuzunguka kisiwa kinachojitawala cha Taiwan, ambacho China inachukulia kuwa sehemu ya ardhi yake. **RFI**

## Waasi DRC wasalimu amri, waondoka eneo mashariki

**Nord Kivu,** DRC

KUNDI la waasi la M23 Movement (M23), linatarajiwa kujiondoa kabisa katika maeneo muhimu katika jimbo la Nord Kivu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wanajeshi wa Kikosi cha Kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF) watachukua maeneo ambayo waasi hao walisalimu amri, ambao kuibuka kwao tena mwishoni mwa mwaka 2021 kumesababisha vifo vya mamia na maelfu ya wengine kuyahama makazi yao.

Mpatanishi maalum wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mzozo wa mashariki mwa DRC, Uhuru Kenyatta, alisema tarehe Aprili 4, mwaka huu, kwamba M23 watajiondoa katika maeneo zaidi ya Nord Kivu kufikia jana.

Hapo awali EAC iliweka kikomo hadi Machi 30 kama siku ya mwisho ya kujiondoa.

Wakati huo huo, duru ya nne ya mazungumzo yenye lengo la kuleta utulivu eneo la mashariki mwa DRC. **BBC**

# TANGULIA 'MFALIME' JUMBE, UMEJITAHIDI KUCHECHEMEA

**Na Saada Akida**

NI mwishoni mwa miaka ya 90 alipozushiwa kifo, hadi akaamua kutunga wimbo wa 'Nachechemea' wakati huo akiitumikia bendi ya Mlimani Park Orchestra, wimbo ambao hadi sasa haujachuja.

Huyu si mwingine bali ni mwimbaji Hussein Jumbe, ambaye alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Amana, Ilala jijini Dar es Salaam na mazishi yake yalitarajiwa kufanyika katika makaburi ya Kisutu jana.

Mwimbaji huyo aliyekuwa na tungo nyingi zenye hisia kali na za visa vingi vya kweli, amefariki huku tungo yake ya mwisho ikiwa ni 'Hasama' iliyoachiwa hewani mwishoni mwa mwaka jana akiwa na bendi ya Mlimani Park Orchestra baada ya kuachana na bendi yake ya Talent.

Wakati wa uhai wake, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa 'Nachechemea' ni wimbo unaotokana na kisa cha kweli, hasa alipougua kwa muda mrefu na kuambiwa kwamba anasumbuliwa na UKIMWI kisha akazushiwa kifo.

Baada ya kupona na kurudi kazini katika bendi yake ya Mlimani, ndipo akafyatua kibao hicho, ili kuonyesha umma wa mashabiki wa muziki wa dansi kuwa yupo na anaendelea kuchechemea.

Wimbo huo ulipendwa na watu wa kada mbalimbali, akiwamo aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mzee Yusuf Makamba, ambaye shughuli za kiserikali akiona bendi hiyo ipo, aliomba kuimbiwa wimbo huo.

Moja ya kauli zake ambayo alikuwa akiirudia mara kwa mara, katika mazungumzo yake, ni kuhusu kisa cha kutunga wimbo wa 'Nachechemea' aliugua sana na kwamba aliponusurika kifo,



asingekufa mapema.

Hata hivyo, amefariki dunia ikiwa imepita zaidi ya miaka 20 tangu alipozushiwa kifo kilichomfanya atunge wimbo huo, unaoendelea kupigwa na bendi ya Mlimani Park, huku sehemu ikiimbwa na Hassan Kunyata.

Katika uhai wake, amewahi kuelezea baadhi ya changamoto alizokutana nazo, ikiwamo kuumwa mara kwa mara magonjwa ya mauzauza, lakini kali zaidi ikiwa ni pale alipoota anapigana na kuku hadi kuvunjika vidole vinne.

Jumbe ameondoka akiwa ameacha umaarufu mkubwa kwenye muziki wa dansi kutokana na tungo zake katika bendi mbalimbali alizowahi kuzitumia kabla ya kujiunga na Sikinde Original, iliotoka ubavuni mwa Mlimani Park.

Baadhi ya tungo zake ni 'Siri ya Nini, Isaya, Huruma kwa Wagonjwa wakati akiwa TOT-Plus, kisha akaurudia wimbo huo akiwa Mlimani Park na kuupa jina la Huruma kwa Wagonjwa na Kilio cha Swahiba'.

Nyimbo nyingine za mkongwe huyo wa muziki wa dansi ni 'Epuka No. 2, Nuru ya Upendo, Shamba, Mtoto wa Mitaani, Chozi la Kejeli', ambazo ni wazi kila mmoja ulitamba kwa wakati wake.

# Mauti yalivyomfika John Bayo

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

ALIYEKUWA Makamu wa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), John Bayo, amefariki dunia.

Katibu wa Kamisheni ya Wanariadha nchini, Andrew Robbi, akizungumza na Nipashe jana, alisema Bayo alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya figo kwa muda mrefu na kumsababishia kutolewa figo moja.

Alisema alianza kusumbuliwa na maradhi hayo tangu Desemba mwaka jana kwa kutibiwa Hospital ya Ocean Road, Dar es Salaam kabla ya Ijumaa iliyopita kwenda Arusha.



"Alikuja Arusha huku akiendelea kujiuguza, lakini jana (juzi) alijisikia vibaya na hali ikazidi kubadilika na kupelekwa katika Hospitall ya Mount Meru kwa ajili ya matibabu na hapo ndipo mauti ilipomkuta," alisema Robbi.

Aidha, taarifa iliyotolewa jana mchana na RT, ilieleza kuwa Bayo alifariki dunia jana jijini Arusha.

Aidha, taarifa hiyo imemwelezea Bayo kuwa ni kati ya mawakala wa kwanza kupeleka wanariadha barani Ulaya kuanzia miaka ya 1980 na ameendelea kuwa nguzo kuu katika uongozi wa mchezo huo hadi mwisho wa uhai wake.

Bayo aliliongoza shirikisho hilo mwaka 2021 akiwa Makamu wa Rais kwa muda wa miezi sita kutoka Januari, hadi alipojiuzulu Agosti, akiwa chini ya Rais wa Shirikisho hilo, Silas Isangi.

Marehemu alikuwa ni mmoja kati ya wataalam wawili wenye kozi ya upimaji wa njia za mbio na kutambulika na Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Riadha (IAAF) akiwa na Daraja B.



Kiungo wa zamani wa Simba, Haruna Moshi 'Boban', akizungumza na waandishi wa habari jana katika Studio za ITV/ Radio One zilizopo Mikocheni, Dar es Salaam, kuhusu mechi yao ya maveteran wa Simba na Yanga itakayopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha mwezi ujao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Simba, Yanga Veteran kukipiga Amri Abeid Arusha

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Televisheni cha ITV/ Radio One kwa kushirikiana na wachezaji wa zamani wa Simba na Yanga, kimeandaa mechi ya mahasimu hao wa jadi inayotarajiwa kupigwa Mei 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam, wachezaji wa timu hizo waliowahi kukipiga miaka ya nyuma, wameahidi kuonyesha uwezo wao waliokuwa wakiuonyesha miaka ya nyuma kwa kuwa vipaji huwa havizeeki.

Kwa upande wa Simba inatarajiwa kuwakilishwa na nyota wengi waliowahi kuichezea kwenye Ligi Kuu na michuano mbalimbali ikiwamo ya kimataifa miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa 2000, ambao ni Lubigisa Madata Lubigisa, Haruna Moshi 'Boban', Joseph Kaniki, Victor Costa, Shekhan Rashid, Athuman Machupa, Duwa Said, Adolf Kondo, Twaha Hamidu na Hamza Maneno.

Wengine ni Amri Kiemba, Clement Kahabuka, Malota Soma, Said Swedi, Jerry Santo, Mark Sirengo, Mashaka Ayubu, Emanuel Gabriel, Boniface Pawassa, Mustapha Hozza, George Masatu na Wyclf Ketto.

Kwa upande wa Yanga, kikosi chao kitakuwa na kina Deo Lucas, Abdul Mtiro, Chibe Chibindu, Issa Kasanga, Mwanamtwa Kihwelo, Kudra Omary, Omega Seme, Athumani Idd 'Chuji', Henry Morris, Semmy Kessy, Sekilojo Chambua, Edibilly Lunyamila, Kenneth Mkapa, Juma Seif 'Kijiko', Stephano Mwasika na Iddi Moshi 'Mnyamwezi'.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika Studio za ITV/ Radio One, Mkurugenzi wa Radio One, Deogratias Rweyunga, alisema veterani hao wanatarajia kukipiga kwenye mchezo utakaopigwa kwa dakika zote 90 ambao kiingilio kitakuwa ni Sh. 5,000.

Alisema maandalizi ya mchezo huo utakaochezwa saa 10 jioni, yapo katika hatua nzuri na tayari wameshawasiliana na uongozi wa Jiji la Arusha kwa ajili ya mechi hiyo na wametoa baraka zote.

"ITV/Radio One tulipokea maombi kutoka kwa wachezaji hawa wa zamani wakiomba kuandaliwa mchezo huu, wakisema wanataka kuonyesha Watanzania namna ambavyo mpira ulivyokuwa unachezwa, ulivyokuwa unapendwa, ili wadau na mashibiki waweze kuwaona," alisema.

Alisema ITV/Radio One itahakikisha mechi hiyo inachezwa kwa viwango vya hali ya juu ambapo itautangaza moja kwa moja na Radio One na kwa wale ambao hawatapata nafasi ya kuiona wataona marudio ITV.

Rweyunga alishukuru Kampuni ya Maji ya Kilimanjaro pamoja na Smart Gin, ambao wameamua kushirikiana nao kudhamini mechi hiyo.

Katibu wa Simba Veteran, Suleiman Mathew, aliishukuru ITV/Radio One kwa kupokea wazo lao na kulifanyia kazi.

"Upande wetu tuko kamili hatujaifanyia masihara mechi hii kwa sababu hatutaki kuwaangusha Wanasimba, timu yetu ipo kamili," alisema.

Mwenyekiti wa Yanga Veteran, David Lihenga, pia aliishukuru ITV/Radio One kwa kukubali kuandaa mechi hiyo na kueleza kwamba maandalizi ya mchezo huo yapo vizuri mpaka sasa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**PHILLIPS AWANIWA VILLA**

ASTON Villa ina nia kubwa ya kusaini mkataba na kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Manchester City. ***(Football Insider)***

**CHILWELL KUSAINI**

KIUNGO wa England, Ben Chilwell, mwenye umri wa miaka 26, yuko tayari kusaini mkataba mpya wa miaka minne katika Klabu ya Chelsea. ***(Athletic)***

**BABA MESSI NA BARCA**

BABA yake Lionel Messi na wakala wake, Jorge alikutana na Barcelona, lakini hakuna pendekezo la uhamisho lililotolewa kwa ajili ya mshambuliaji huyo Muargentina mwenye umri wa miaka 35. ***(Cadena Ser, via Mirror)***

**REUS MKATABA MPYA**

WINGA wa Ujerumani, Marco Reus mwenye umri wa miaka 33, yuko tayari kusaini mkataba mpya na Borussia Dortmund, lakini mshahara wake utakatwa ili aendelee kubaki katika klabu hiyo. ***(Bild)***

**WAN-BISSAKA AWANIWA**

KLABU ya West Ham inamfuatilia kwa karibu mchezaji Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 25, wakiwa na mpango wa kumsajili msimu ujao wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**BALOGUN SOKONI ARSENAL**

ARSENAL iko huru kumuuza mshambuliaji wa kikosi cha England, Folarin Balogun, kwa msimu ujao. Kijana huyo mwenye umri wa miaka 21, kwa sasa yuko katika klabu ya Reims kwa mkataba wa mkopo. ***(Times)***

**ARSENAL, CHELSEA KWA BAKU**

ARSENAL na Chelsea ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazotaka kumsajili kiungo wa Wolfsburg na Ujerumani, Ridle Baku, 25. ***(Bild)***

**FELIX KUBAKI CHELSEA**

CHELSEA ina matumaini ya kuendelea kuwa na Joao Felix msimu ujao. 'The Blues' hao walisaini mkataba wa mkopo na mshambuliaji huyu Mreno mwenye umri wa miaka 23, kutoka Klabu ya Atletico Madrid, Januari, mwaka huu. ***(Fabrizio Romano)***

**PEDRO ATAKIWA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle United inataka kusaini mkataba na mshambuliaji Mbrazili Joao Pedro mwenye umri wa miaka 21, kutoka Watford katika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**FERGUSON NA MKATABA**

KLABU ya Brighton ina matumaini ya kumpa mkataba mpya Evan Ferguson licha Manchester United na Tottenham Hotspur kuwa na nia ya kumsajili. ***(Mail)***

**RABIOT AISIKILIZIA JUVE**

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28, amesema bado anasubiri iwapo atasaini mkataba mpya na Juventus. Mkataba wake unaomalizika msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI SASA AJIVUNIA UIMARA WA BARCA KILELENI LALIGA

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amekiri kuwa Barcelona ipo katika "hali nzuri sana" kwenye kilele cha Ligi Kuu Hispania, LaLiga, lakini ameachwa akijutia kukosa ushindi nyumbani dhidi ya Girona Jumatatu.

**'The Blaugrana' hao wangeweza kusonga mbele kwa pointi 15 kwa ushindi, baada ya Real Madrid kushindwa 3-2 dhidi ya Villarreal Jumapili, lakini ilibidi watoe nafasi ya kuongoza kwa pointi 13 baada ya sare tasa pale Camp Nou.**

Ilikuwa sare ya pili kwa Barca bila kufunga Camp Nou katika LaLiga msimu huu, kama vile katika kampeni zao nne za awali za ligi zikijumulishwa, baada ya kipa wa Girona, Paulo Gazzaniga kuonesha kiwango kizuri.

Kocha Mkuu wa Barca, Xavi amesema walikuwa nafasi ya kupata ushindi, ingawa alikataa kuikosoa timu yake kwa sare hiyo.

Alipoulizwa na DAZN kama ilikuwa nafasi ya kujutia, Xavi alijibu: "Hatuwezi kuwa na uhakika na pointi moja nyumbani, lakini tuna pointi 13 mbele ya nafasi ya pili zikiwa zimesalia mechi 10.

"Tupo katika hali nzuri sana, tumejaribu, tumecheza mchezo sahihi, tumepata nafasi nyingi za kufunga na kushinda mchezo dhidi ya timu nzuri sana.

"Tulikosa tu kupata bao la kwanza. Nadhani tulistahili kushinda."

Barca waliendelea na msururu wao wa kutopoteza nyumbani katika LaLiga katika kampeni hii (mechi 14), huku Union Berlin na Bayern Munich pekee zikijivunia rekodi kama hiyo ya msimu mzima katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu."

> ●●● Tupo katika hali nzuri sana, tumejaribu, tumecheza mchezo sahihi, kufunga na kushinda...

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,102,0

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 12 NA 13 APRILI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/04/23 | 22:00 | AC Milan vs Napoli | 2.64 | 3.08 | 2.59 |
| 02. 12/04/23 | 22:30 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 2.75 | 2.65 | 2.49 |
| 03. 12/04/23 | 23:30 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pereira | 2.23 | 2.95 | 3.21 |
| 04. 13/04/23 | 01:00 | Coritiba vs Sport Recife | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 13/04/23 | 01:00 | Belgrano Cordoba vs Huracan | 2.86 | 2.75 | 2.59 |
| 06. 13/04/23 | 03:30 | Rosario Central vs Independiente | 2.49 | 2.65 | 2.75 |
| 07. 13/04/23 | 03:30 | Estudiantes LP vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.91 | 3.32 |
| 08. 13/04/23 | 05:05 | Correcaminos Uat vs Club Celaya | 2.57 | 3.07 | 2.60 |
| 09. 13/04/23 | 19:45 | Feyenoord vs Roma | 2.24 | 3.14 | 3.19 |
| 10. 13/04/23 | 20:30 | Altay vs Altinordu | 2.18 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 13/04/23 | 22:00 | Anderlecht vs AZ Alkmaar | 2.65 | 3.21 | 2.55 |
| 12. 13/04/23 | 22:30 | Colon Santa Fe vs Talleres | 2.65 | 2.80 | 2.44 |
| 13. 13/04/23 | 23:30 | Envigado FC vs Deportes Tolima | 2.75 | 2.70 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CARRAGHER: HAKUNA BEKI BORA KAMA VAN DIJK



**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk huenda hajawa kwenye kiwango bora msimu huu, lakini Jamie Carragher amesema hakuna beki wa kati katika Ligi Kuu England ambaye amewahi kuwa na mchango mkubwa kwa timu yao kama yeye.

Carragher alimtetea kwenye Twitter, akipendekeza Van Dijk alikuwa bora zaidi kuliko mlinzi wa zamani wa Manchester United, Nemanja Vidic, na alikuwa amefika kiwango sawa na Kevin De Bruyne katika miaka ya hivi karibuni.

Hilo lilikuja baada ya Liverpool kutoka sare ya mabao 2-2 na Arsenal kwenye Uwanja wa Anfield Jumapili, wakati safu ya ulinzi ya Jurgen Klopp ilipoonekana kupwaya huku Gabriel Martinelli na Gabriel Jesus wakipachika mabao.

Uchezaji wa Van Dijk umetiliwa shaka mara kwa mara msimu huu, huku Carragher akitoa tathmini kali ya beki huyo baada ya Liverpool kuchapwa mabao 5-2 na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Februari mwaka huu.

Wakati nahodha wa zamani wa Liverpool, Carragher alikiri hali ya kukatisha tamaa ya msimu wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, anaamini hakuna beki wa kati anayekaribiana na Van Dijk katika enzi hii ya Ligi Kuu England.

Carragher aliandika: "VVD (Van Dijk) ni bora zaidi kuliko Vidic.



## *Son aelezea sababu kushuka kiwang*

**LONDON,** England

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Heung-Min Son, amekiri kuhisi presha zaidi baada ya kushinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England kama mfungaji bora msimu uliopita.

Son aliifungia Spurs mabao 23 ya ligi wakati wa msimu wa 2021-22, akimaliza akiwa sawa na Mohamed Salah kama mfungaji bora.

Hayo yalikuwa jumla ya mabao bora zaidi ya Son ya Ligi Kuu kwa msimu mmoja, sita zaidi ya mabao 17 aliyofunga miezi 12 mapema, na anaamini kwamba matokeo kama hayo yalileta presha ya kiwango ambacho hakuwahi kuhisi hapo awali.

Ingawa alisisitiza kuwa anapenda shinikizo, kiwango cha mchezaji huyo huku kukiwa na kutambulika zaidi kimekuwa hafifu, akifunga mabao saba pekee ya Ligi Kuu katika mechi 28 alizocheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, bado ana mechi nane nyingine za kucheza msimu huu, na alifunga katika ushindi wa mabao 2-1 Jumamosi dhidi ya Brighton.

Lakini bila kujali jinsi 2022-23 itaisha, Son hao sababu kwa nini hawe kurejea akiwa na nguv zaidi msimu ujao.

Son aliwaamb waandishi wa habari; "A galia, ikiwa ninataka k toa visingizio kwa jinsi n ivyocheza, naweza kupa vingi, lakini mimi si ai ya mtu anayezunguka n kusema, 'huyo hakuw mimi halisi. Ninakubali s kuwa katika kiwango ch juu."

"Msimu uliopita u kuwa mzuri na kushinc Kiatu cha Dhahabu i kuwa wakati wa ajab ambao ulinipa ujasiri w ajabu.

082,037/-

# RAIS SAMIA AIPA MAMILIONI FOUNTAIN GATE UBINGWA CAF

**Na Saada Akida**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ameipongeza timu ya wasichana ya mpira wa miguu ya Sekondari ya Fountain Gate kutoka Dodoma, kwa kutwaa ubingwa wa mashindano ya soka kwa Shule za Sekondari ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF African Schools Football Championship Continental) kwa wasichana.

**Pongezi hizo ni baada ya timu hiyo ya wasichana ya Fountain Gate kuibuka na ubingwa wa michuano hiyo inayoandaliwa na CAF, kwa kushinda mabao 3-0 dhidi ya Ecole Omar IBN Khatab kutoka Morocco katika fainali iliyochezwa Jumamosi iliyopita nchini Afrika Kusini.**

Ushindi huo unaifanya Fountain Gate kuvuna kitita cha Dola 300,000 sawa na Sh. milioni 701.2 kama mabingwa wa mashindano hayo Afrika.

Kupitia ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Rais Samia, alisema ushindi wao unakwenda sambamba na nia ya serikali kuendelea kuboresha mtaala wa elimu yetu katika kukutaza si tu elimu ya darasani, bali pia ya vipaji, kupata watu zaidi wenye uwezo wa kutumia maeneo hayo mawili kuleta maendeleo.

Wakati huo huo, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema Rais Samia kupitia wizara hiyo amewapongeza na kuwapa zawadi ya Sh. milioni 10 kwa wachezaji na benchi la ufundi wa mabingwa hao wa Afrika.

Mbali na zawadi hiyo, timu hiyo imepata mwaliko muhimu kutoka kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, wa kutembelea Bungeni, Dodoma Alhamisi wiki hii.

Alisema kufanya vizuri katika sekta ya michezo serikali kupitia wizara husika wanaenda kukaa na Wizara ya Elimu kuweka mtaala wa michezo shuleni kuwapo na somo maalum.

"Isiishie katika kusoma tu, bali litawekwa kwenye mitihani na kufanywa kama ilivyo kwa masomo mengine, pia tumezitaka kila shule ziwe na sehemu ya michezo ili kupata nafasi ya kuendeleza vipaji kuanzia shuleni," alisema na aliongeza.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema kitendo cha timu ya Fountain Gate kutwaa ubingwa huo wa Afrika ni rekodi ya pili kwa kipindi cha Rais Samia.

Alisema rekodi ya kwanza ni timu ya U-17, wasichana kucheza Kombe la Dunia na timu ya Wanawake ya Faountain Gate kutwaa ubingwa wa Afrika inakuwa ya pili chini ya Dk. Samia.

Naye Mkurugezi wa Fountain Gate, Japhet Makau, alisema baada ya kukabidhiwa bendera walikuwa na jukumu zito kwa mechi ya kwanza dhidi ya wenyeji, Afrika Kusini.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana, akipokea Kombe la Mabingwa wa Afrika kwa Shule za Sekondari kutoka kwa Nahodha wa Timu ya Fountain Gate, Beatrice Charles, ambao walikuwa wawakilishi wa Tanzania katika mashindano hayo yaliyomalizika wiki iliyopita nchini Afrika Kusini. Hafla hiyo ilifanyika Dar es Salaam jana, kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayai. **MPIGAPICHA WETU**

# *Baleke: Kiwango changu bado*

INATOKA UKURASA 24

wa kuendelea kuzoea mazingira ya ligi ya Tanzania, hivyo anatarajia msimu ujao kwake na Simba utakuwa mzuri zaidi.

Aliongeza kwa sasa nguvu kubwa ni kuangalia yaliyopo mbele hususan mechi zilizosalia katika ligi ikiwamo mchezo wa 'dabi' dhidi ya Yanga Jumapili wiki hii, Kombe la Shirikisho na kazi kubwa kwao ni kuelekea mchezo wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.

"Mbele yetu tuna kazi nyingi, tunapaswa kuelekeza nguvu kupambana kwa pamoja kwa kushinda mechi zetu zijazo dhidi ya Yanga, kutinga hatua ya nusu fainali ya CAF na tunapaswa kuongeza ushindani zaidi tufanikiwe, malengo yetu hayo," alisema Baleke ambaye ameanza kuzua hofu kwa wapinzani hasa kwa kasi yake ya kufunga.

Baleke aliyesajili Simba kipindi cha dirisha dogo msimu huu, hadi sasa amefunga mabao 14 tangu ajiunge na timu hiyo, huku akiwa amefikisha saba kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, matano kwenye Kombe la FA na matatu Ligi ya Mabingwa Afrika.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/04/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Brentford FC | 2.33 | 3.10 | 2.95 |
| 02. 15/04/23 | 17:00 | Chelsea FC vs Brighton & Hove Albion | 2.41 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 15/04/23 | 17:00 | Southampton FC vs Crystal Palace | 2.60 | 3.10 | 2.60 |
| 04. 15/04/23 | 17:00 | Blackpool vs Wigan Athletic | 2.35 | 3.05 | 3.00 |
| 05. 15/04/23 | 17:00 | Queens Park Rangers vs Coventry City | 2.90 | 3.00 | 2.41 |
| 06. 15/04/23 | 17:00 | Stoke City vs West Bromwich Albion | 2.55 | 3.10 | 2.65 |
| 07. 15/04/23 | 17:00 | KAS Eupen vs SV Zulte Waregem | 2.33 | 3.40 | 2.75 |
| 08. 15/04/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Portimonense SC | 2.38 | 3.00 | 3.00 |
| 09. 15/04/23 | 18:00 | Stade Rennes vs Stade Reims | 2.22 | 3.30 | 2.95 |
| 10. 15/04/23 | 19:15 | KV Oostende vs Oud-Heverlee Leuven | 2.48 | 3.45 | 2.50 |
| 11. 15/04/23 | 22:00 | Sparta Rotterdam vs SC Heerenveen | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 12. 15/04/23 | 22:00 | America FC MG vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 13. 16/04/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Sao Paulo FC SP | 2.49 | 3.05 | 2.80 |
| 14. 16/04/23 | 03:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Belgrano | 2.30 | 2.75 | 2.90 |
| 15. 16/04/23 | 19:30 | Malaga CF vs FC Cartagena | 2.31 | 2.90 | 3.20 |
| 16. 16/04/23 | 20:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.60 | 2.85 | 2.47 |
| 17. 16/04/23 | 20:30 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.75 | 3.35 | 2.32 |


## MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JAMATANO - 12/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1968 | Chungnam Asan vs Jeonnam Dragons | 2.20 | 2.95 | 3.26 |
| 13:00 | 2397 | Sangju Sangmu vs Seongnam Ilhwa | 1.97 | 3.11 | 3.68 |
| 14:00 | 1313 | FK Lviv vs Shakhtar Donetsk | 19.49 | 6.77 | 1.10 |
| 14:00 | 5488 | SHB DA Nang vs CLB Viettel | 4.20 | 2.97 | 1.87 |
| 14:00 | 5630 | Magara Young Boys vs Le Messager Ngozi | 3.05 | 3.05 | 2.07 |
| 15:00 | 2489 | WIT Georgia vs Loko Tbilisi | 1.95 | 3.25 | 3.10 |
| 15:00 | 5936 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs Merani Martvili | 3.31 | 3.46 | 1.96 |
| 15:30 | 1370 | Geylang Int. vs Balestier Khalsa | 1.57 | 4.32 | 4.11 |
| 16:00 | 4578 | Unia Skierniewice vs Concordia Elblag | 1.64 | 3.74 | 4.47 |
| 16:00 | 4733 | Manisa BBSK vs Bandirmaspor | 1.96 | 3.45 | 3.24 |
| 16:00 | 5356 | Burundi Sport Dynamic vs Olympic Star | 2.65 | 2.75 | 2.50 |
| 16:30 | 1311 | Holy Ghost vs Gaborone United | 8.28 | 5.17 | 1.27 |
| 16:30 | 1823 | Orapa United vs Mogoditshane Fighters | 1.22 | 5.39 | 10.36 |
| 16:30 | 2300 | Bali Utd Pusam vs Psis Semarang | 1.50 | 4.20 | 4.92 |
| 16:30 | 5983 | Police XI vs Township Rollers | 3.64 | 3.22 | 1.94 |
| 17:00 | 2187 | FK Graficar Beograd vs Metalac | 1.76 | 3.38 | 4.05 |
| 17:00 | 3691 | Bekescsabai Elore vs Csakvari TK | 2.43 | 2.90 | 2.60 |
| 17:00 | 3730 | Dorogi FC vs Nyiregyhaza | 2.27 | 3.04 | 2.94 |
| 17:00 | 4990 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Imt Novi Beograd | 2.20 | 3.02 | 3.07 |
| 17:00 | 5233 | FK Jedinstvo UB vs FK Radnicki Sremska Mitrovica | 2.28 | 2.83 | 3.14 |
| 17:00 | 5603 | Anorthosis Famagusta vs Akritas Chlorakas | 1.33 | 4.73 | 8.40 |
| 17:00 | 5957 | Radnicki Nis vs Javor Ivanjica | 1.78 | 3.23 | 4.21 |
| 17:00 | 5988 | Gyirmot FC vs Bgsz Siofok | 1.56 | 3.75 | 4.93 |
| 17:15 | 3695 | Olympiacos Piraeus B vs Episkopi FC | 1.45 | 3.78 | 6.84 |
| 18:00 | 4546 | Mkp Carina Gubin vs MKS Kluczbork | 2.20 | 3.10 | 2.75 |
| 18:30 | 1992 | Slaven Belupo vs Hajduk Split | 3.33 | 3.33 | 2.01 |
| 19:00 | 1095 | FK Trajal vs Macva Sabac | 1.97 | 2.78 | 4.11 |
| 19:00 | 1644 | Sporting Lisbon B vs Vitoria Setubal | 1.88 | 3.47 | 3.57 |
| 19:00 | 1655 | Pecs MFC vs Duna Aszfalt Tvse | 1.67 | 3.20 | 4.40 |
| 19:00 | 1688 | AB Argir vs KI Klaksvik | 13.00 | 6.60 | 1.09 |
| 19:00 | 2495 | Sloboda vs Indjija | 2.37 | 2.88 | 2.93 |
| 19:00 | 2679 | Szeged vs FC Ajka | 2.19 | 2.85 | 3.00 |
| 19:00 | 2682 | Dinamo Batumi vs Dinamo Tbilisi | 2.08 | 3.10 | 3.00 |
| 19:00 | 2745 | Slovan Bratislava vs MFK Skalica | 1.20 | 6.19 | 9.70 |
| 19:00 | 3911 | Nieciecza KS vs Puszcza Niepolomice | 1.87 | 3.38 | 3.59 |
| 19:00 | 5515 | Radnik Surduluca vs FK Napredak | 2.32 | 2.87 | 3.03 |
| 19:30 | 5001 | Olympiakos vs AEK Athens | 2.30 | 3.17 | 2.85 |
| 20:30 | 1850 | Eyupspor vs Genclerbirligi | 1.49 | 3.96 | 5.35 |
| 20:30 | 2872 | Marumo Gallants FC vs Chippa Utd | 2.62 | 2.83 | 2.83 |
| 20:30 | 5827 | Golden Arrows vs Mamelodi Sundowns | 5.23 | 3.45 | 1.64 |
| 21:30 | 5911 | Nacional Madeira vs Sporting Braga | 5.18 | 3.73 | 1.56 |
| 21:45 | 1741 | Eastleigh vs Gateshead | 2.39 | 3.26 | 2.79 |
| 21:45 | 3999 | Linfield Belfast vs Glentoran Belfast | 2.04 | 3.03 | 3.44 |
| 22:00 | 4006 | AC Milan vs Napoli | 2.65 | 3.04 | 2.61 |
| 22:00 | 5141 | Real Madrid vs Chelsea | 1.72 | 3.49 | 4.49 |
| 22:15 | 3163 | Ghazl EL Mahallah vs Coca Cola | 5.21 | 3.35 | 1.68 |
| 22:15 | 5893 | El Daklyeh vs Ceramica Cleopatra | 4.64 | 2.77 | 1.97 |
| 22:30 | 2842 | Nova Iguacu RJ vs America Mineiro MG | 4.46 | 3.27 | 1.75 |
| 22:30 | 4934 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 2.51 | 2.90 | 2.80 |
| 23:30 | 5383 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pereira | 2.54 | 3.11 | 2.59 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Aprili 12, 2023
Nipashe



**Mauti yalivyomfika John Bayo** UKURASA 20

**BINJUKA...**



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, akibinjuka (acrobatic), kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ihefu FC, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya. **MPIGAPICHA WETU**

## Tangulia 'mfalme' Jumbe, umejitahidi kuchechemea

**Na Sabato Kasika**

NI mwishoni mwa miaka ya 90 alipozushiwa kifo, hadi akaamua kutunga wimbo wa 'Nachechemea' wakati huo akiitumikia bendi ya Mlimani Park Orchestra, wimbo ambao hadi sasa haujachuja. Huyu si mwingine bali ni...



HABARI UKURASA 20

## Simba, Yanga Veteran kukipiga Amri Abeid Arusha

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Televisheni cha ITV/Radio One kwa kushirikiana na wachezaji wa zamani wa Simba na Yanga, kimeandaa mechi ya mahasimu hao wa jadi inayotarajiwa kupigwa Mei 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha...



HABARI UKURASA 20

# Baleke: Kiwango changu bado

## ● ● ● Aitaja mechi na Yanga, Simba yaweka wazi mkataba wake yasema yupo sana hadi...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, akieleza bado hajarejea katika ubora wake wa kufumania nyavu na kwamba anahitaji kupata muda wa kuendelea kuonesha kiwango kizuri zaidi, uongozi wa klabu hiyo umewatoa hofu mashabiki wake kuhusu mkataba wa straika huyo na kusema bado yupo sana.

Baleke ambaye alifunga mabao mawili wakati wakishinda 2-0 juzi katika Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC, amekuwa akidaiwa kuwa yupo Simba kwa mkopo na mwishoni mwa msimu Klabu yake ya TP Mazembe imeeleza nia yake ya kumrejesha.

Hata hivyo, uongozi wa Klabu ya Simba umeliambia Nipashe jana kuwa ina mkataba naye hadi Desemba 2024 na wala hayupo kwa mkopo kama baadhi ya watu wanavyodhani.

**Straika huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo amewafunga Ihefu mabao matano ndani ya siku chache, kwani Ijumaa iliyopita aliifunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa, Uwanja wa Azam Complex, Simba ikishinda mabao 5-1.**

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amezima minong'ono kuwa mchezaji huyo yupo kwa mkopo, akisema Simba imempa mkataba wa miaka miwili ambao utamalizika Desemba 2024.

"Desemba mwaka jana tumemsainisha kutoka TP Mazembe kwa mkataba wa miaka miwili, kutoka Desemba hadi sasa ni miezi minne tu, kwa hiyo katika mkataba wa miezi 24, Baleke ametumia miezi hiyo tu, hivyo amesalia na miezi 20 mkononi, wanachama na mashabiki wa Simba watulie, waendelee kufurahia mema ya straika huyo.

"Uwapo wake na wale wenye wasiwasi kukutana naye kiasi cha kupiga simu asubuhi mchana na usiku TP Mazembe kumuulizia Baleke, tuwaambie tu kuwa ni mchezaji wetu kwa miaka miwili, rasmi leo Klabu ya Simba tunaweka wazi kuwa tuna mkataba naye wa miaka hiyo na wala si kwa miezi sita kama wengine wanavyodai, tulisaini naye mkataba kutoka Desemba 2022, ambao utaisha Desemba 2024," alisema Ahmed.

Kwa upande wa Baleke akizungumza na gazeti hili jana, alisema bado hajaanza kuzoea vizuri ligi na ana imani kila muda unavyozidi kwenda na kupata nafasi ya kucheza ndani atazidi kuwa bora.

Alisema kufunga ni jukumu lake kila anapopata nafasi ya kufanya hivyo na kwamba wanacheza watu wengi uwanjani, hivyo akiona mchezaji mwenzake yupo nafasi nzuri ya kufunga anatoa pasi.

"Tunajua wote tunajenga Simba moja, hutakiwi kuwa mchoyo, mchezaji mwenzako anapokuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuisaidia timu kupata ushindi unamsaidia kwa sababu ninaamini tuliokuwapo hapa tunahitaji kufikia malengo," alisema.

Alisema anaamini kwa sasa tayari ameanza kuzoea mfumo na bado anahitaji muda kidogo

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >